

**MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA**



Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

# **TAARIFA YA UTENDAJI KAZI 2020/21**



**Septemba, 2021**

### **Dhima**

Kulinda afya ya jamii  
kwa kuzuia athari  
zinazoweza kujitokeza  
kutokana na matumizi  
ya chakula, dawa,  
vipodozi na vifaa tiba

### **Dira**

Kuwa Mamlaka  
inayoongoza barani  
Afrika katika kudhibiti  
usalama, ubora na  
ufanisi wa chakula,  
dawa, vipodozi na  
vifaa tiba kwa wote.

### **Falsafa**

Kutoa huduma za  
udhibiti katika kulinda  
afya ya jamii na  
mazingira kwa  
kutumia wafanyakazi  
wenye ujuzi na ari ya  
kazi.

### **Misingi ya kazi**

- Kufanya kazi kwa ushirikiano
- Uaminifu
- Kuzingatia mahitaji ya wateja
- Ubora
- Uwajibikaji

## BARUA YA KUWASILISHA



**Mhe. Dkt. Doroth Gwajima (MB),**  
Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii,  
Jinsia, Wazee na Watoto,  
Mji wa Serikali, Barabara ya afya,  
S.L.P 743,  
11478 Dodoma.



**Prof. Abel Makubi,**  
Katibu Mkuu (Afya),  
Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii,  
Jinsia, Wazee na Watoto,  
Mji wa Serikali, Barabara ya afya,  
S.L.P 7433,  
11478 Dodoma.

Mhe. Waziri,

Ninayo heshima kubwa kuwasilisha kwako Taarifa ya Utendaji Kazi ya Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) kwa kipindi cha mwaka 2020/21.

Taarifa hii imeeleza hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa shughuli za udhibiti wa ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa lengo la Kulinda Afya ya Jamii.

Nawasilisha.

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'Abel Makubi'.

Prof. Abel Makubi

**KATIBU MKUU (AFYA)**

## MAELEZO YA MWENYEKITI WA BODI YA USHAURI (MAB)

Taarifa hii ya utendaji kazi kwa mwaka wa fedha 2020/21 inaainisha kazi na majukumu yaliyotekelezwa na Mamlaka katoika kutekeleza jukumu lake la msingi la kulinda afya ya jamii. Vilevile maeneo yanayohitaji kupewa kupaumbele ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wake wa majukumu yameinishwa katika taarifa hii .

Mwaka 2020/21 ni mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa Mpango mkakati wa TMDA wa miaka mitano (5) 2017/18 - 2020/21 ambao ulifanyiwa mapitio mwaka 2020 wenye lengo la kuimarisha utekelezaji wa shughuli za kudhibiti usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

Katika mwaka huu, Mamalaka imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kudhibiti ubora usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Aidha kuanzia mwezi Aprili, 2021 Mhe. Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto amekasimisha jukumu la udhibiti wa bidhaa za tumbaku kwa TMDA jukumu ambalo limeanza kutekelezwa.

TMDA imeendelea kushikilia cheti cha ithibati kwa kiwango cha ISO 9001: 2015 baada ya kukidhi vigezo kufuatia kaguzi zilizofanyika. Hii imechangiwa na jitahada zinazofanywa katika kuboresha mifumo ya utoaji huduma sambamba na utekelezaji wa mifumo bora ya Utendaji Kazi (Quality Management System) katika kutoa huduma. Aidha huduma za TMDA zimeendelea kutolewa kwa kuzingatia viwango vya utoaji huduma vilivyoinishwa katika Mkataba wa Huduma kwa Wateja (CSC) 2020 ili kukidhi mahitaji na matarajio ya wateja.

Taasisi imeendelea kuimrisha shughuli za uchunguzi wa kimaabara kwa kufanya uwekezaji katika ununuzi wa vifaa vya kisasa pamoja na kuwajengea uwezo wataalamu wa maabara. TMDA imekamilisha ujenzi wa jengo la maabara ya Kanda ya kati Dodoma na hivi sasa mchakato wa manunuzi ya vifaa unaendelea na maabara hii itakuwa mahususi kwa ajili ya upimaji wa sampuli za bidhaa za tumbaku.

Matumizi na usimamizi wa rasilimali za Mamlaka pamoja na utoaji huduma umeendelea kuzingatia mifumo bora ya kiutendaji, Sheria, Kanuni na taratibu ambapo hesabu za fedha na rasilimali za TMDA kwa kipindi kinachoishia Juni, 2021 zipo tayari kwa ukaguzi unaofanywa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).



TMDA imeendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali ya wadau kuhusu kazi na majukumu yake katika kulinda afya ya jamii. Uhamasishaji umejikita katika utoaji wa taarifa za madhara au maudhi yanayotokana na matumizi ya dawa za chanjo pamoja na matumizi sahihih ya dawa na vifaa tiba ili kuwa na taarifa sahihi kuhusu usalama ubora na ufanisi wa bidhaa zinazodhibitiwa

Kwa niaba ya MAB naipongeza Menejimenti pamoja na watumishi wote kwa kufanya kazi kwa weledi na kujituma katika kuhakikisha kuwa bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi vilivyo katika soko ni bora, salama na fanisi. Vilevile, natoa shukrani kwa wadau wote wa TMDA pamoja na wananchi kwa ujumla kwa ushirikiano wao katika kusaidia Mamlaka kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Aidha, natoa rai kwa wadau wote kutekeleza wajibu wao ipasavyo katika kuhakikisha kuwa bidhaa za, dawa, vifaa tiba na vitendanishi vilivyopo katika soko vinakidhi vigezo vya usalama, ubora na ufanisi.

Bodi ya Ushauri (MAB) chini ya uenyekiti wangu itaendelea kutoa maelekezo kwa Menejimenti ya TMDA sanjari na ushauri kwa Wizara katika kuwahakikishia kuwa dawa, vifaa tiba na vitendanishi vilivyopo katika soko la Tanzania ni salama, bora na vyenye ufanisi.

**Eric Shitindi**

**MWENYEKITI WA BODI YA USHAURI**

## MAELEZO YA MKURUGENZI MKUU

TMDA inatekeleza majukumu yake chini ya Mpango Mkakati wake wa miaka mitano 2017/18 ambao ulirejewa mwaka 2020 kutokana na mabadiliko ya kimajukumu ya iliyokuwa TFDA ambapo udhibiti wa bidhaa za chakula na dawa ulitenganishwa.

Taarifa hii ya mwaka wa fedha 2020/21 inaainisha hatua iliyofikiwa na Mamlaka katika utekelezaji wa kazi na majukumu yake ya kudhibiti ubora usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi nchini. Aidha, maeneo yanayohitaji kupewa kipaumbele katika mwaka ujao yameanishwa.

Huu ni mwaka wa mwisho wa utekelezaji wa mpango mkakati wa awamu ya nne wenye miaka mitano (2017/18-2021/22) wenye malengo mkakati saba (7) ambapo kumekuwa na mafanikio makubwa katika utekelezaji wake.

Katika kuimarisha udhibiti wa ubora usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi, jumla ya maombi 1,302 ya usajili wa dawa za binadamu yalipokelewa na 1,214 (94%) kutathminiwa ambapo 1,111 (85%) yaliidhinishwa baada ya kukidhi vigezo. Aidha, maombi 163 ya usajili wa dawa za mifugo yalipokelewa na 148 (91%) kati ya hayo yalitathminiwa na 83 yalilikidhi vigezo na kuidhinishwa.

Jumla ya Maombi 377 ya usajili wa vifaa tiba na 169 ya vitendanishi yalipokelewa na kati ya hayo 324 (86%) na 162 (96%) ya vitendanishi yalifanyiwa kazi. Kati ya maombi ya usajili wa vifaa tiba na vitendanishi maombi 317 ya vifaa tiba na 124 ya vitendanishi yalilikidhi vigezo na kuidhinishwa.

Vilevile, Mamlaka ilipokea maombi 3,353 ya usajili wa bidhaa za chakula ambapo yote (100%) yalifanyiwa tathmini. Maombi 2,876 (86%) kati ya yaliyofanyiwa tathmini yaliidhinishwa. Idadi ya maombi ya usajili yaliyoidhinishwa imeongezeka kutoka 2,104 mwaka 2017/18 hadi kufikia 2,876 kwa mwaka 2018/19 ikiwa ni ongezeko la maombi 772. Ongezeko hilo linatokana na kuimarika kwa shughuli za udhibiti na utii wa sheria bila shuruti miongoni mwa wafanyabiashara.

Aidha, jumla ya maombi 679 ya usajili wa maeneo ya biashara yalipokelewa katika kipindi tajwa ambapo 671 (99%) yalifanyiwa kazi na kati ya hayo maeneo 629 (94%) yalilikidhi vigezo na kusajiliwa. Majengo yasiokidhi vigezo vya usajili wamiliki walipatiwa maelekezo ya kufanya marekebisho katika maeneo hayo.

Mamlaka pia ilipokea maombi 13,003 ya vibali vya kuingiza bidhaa nchini na 1,467 vya kusafirisha bidhaa nje ya nchi kati ya hayo maombi 11,901 ya kusafirishakuingiza bidhaa nchini na 1,358 yalilikidhi vigezo na kutolewa vibali. Aidha vibali 21,211 vya kuingiza bidhaa nchini na 1,340 vya kusafirisha bidhaa nje ya nchi vilikaguliwa katika vituo mbalimbali vya forodha.

Mamlaka ilifanya ukaguzi wa maeneo 10,846 ya biashara ya bidhaa zinazodhibitiwa na Mamlaka ambapo maeneo 8,364 sawa na 77% yalilikidhi vigezo. Kiwango hiki cha kukidhi vigezo vya viwanda na



maeneo ya biashara kinatoa picha kuwa bidhaa zinazalishwa na kuuzwa katika mazingira bora na salama kwa watumiaji.

Kwa upande wa huduma za maabara, jumla ya sampuli 3,913 zilipokelewa katika maabara ambapo sampuli 3,603 (92%) zilichunguzwa na 3,179 (88%) zilifaulu. Aidha, katika kuhakikisha kwamba viwango vya ISO /IEC 17025:2005 na WHO/GLP vinafuatwa na kutekelezwa, Mamlaka ilikaguliwa na bodi ya ithibati SADCAS/SANAS, matarajio ni kuendelea kushikilia cheti hicho cha ithibati.

Elimu kwa umma ilitolewa kwa makundi mbalimbali ya wananchi pamoja na kutangaza huduma za Mamlaka kupitia njia mbalimbali za uelimishaji. Njia zilizotumika ni pamoja na kufanya mihadhara (Outreach Campaigns) ambapo zaidi ya watu 283,160 walifikiwa, kurusha matangazo mafupi ya uelimishaji kupitia vituo vya runinga na redio na kushiriki katika maonesho mbali mbali.

Kuhusu matumizi na usimamizi wa rasilimali, Jumla ya TZS 35.5 bilioni zilikusanywa sawa na 100% ya bajeti ya makusanyo ya TZS 35.5 bilioni ya mwaka 2020/21. Kati ya hizo TZS 31.3 (88%) ni ada na tozo, TZS 3.6 bilioni sawa na (10%) ni mchango wa Serikali kuu na TZS 554 milioni (2%) ni fedha za Washirika wa Maendeleo. Mamlaka ilitumia jumla ya TZS 37.5 bilioni sawa na 91% ya bajeti ya matumizi iliyopangwa mwaka huu ambayo ni TZS 41 bilioni.

Kwa ujumla Malengo Mkakati ya TMDA yametokelezwa kwa ufanisi na mafanikio makubwa sambamba na utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa kupambana na kuzuia rushwa.

Ni dhahiri kuwa mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka umetokana na watumishi kufanya kazi kwa moyo juhudi na kujituma. Nachukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza watumishi wote na nawaomba wazidi kuwa na ari na ushirikiano. Aidha, shukrani za dhati ziende kwa Mwenyekiti na wajumbe wa MAB kwa maelekezo yao yaliyowezesha utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka kwa ufanisi.

Adam M. Fimbo

**MKURUGENZI MKUU**

## TAARIFA KAMILI

### 1. UTANGULIZI

Katika kipindi cha mwaka 2020/21, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) iliendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mpango kazi na Bajeti ya mwaka 2020/21 iliyoidhinishwa. Taarifa hii inaainisha kazi zilizotekelezwa kwa kipindi tajwa kwa kuzingatia malengo mkakati saba (7) ya Mpango Mkakati wa Mamlaka (2017/18 - 2021/22) ambayo ni: -

- i) Kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi;
- ii) Kuboresha huduma za maabara;
- iii) Kuimarisha utoaji elimu kwa umma na kuboresha huduma kwa wateja;
- iv) Kuimarisha uwezo wa Mamlaka katika kutoa huduma za udhibiti;
- v) Kupunguza maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na kuboresha huduma kwa waathirika wa UKIMWI na wenye magonjwa yasiyoambukiza;
- vi) Kuimarisha na kutekeleza kwa ufanisi Mkakati wa Taifa wa kupambana na kuzuia rushwa; na
- vii) Kuboresha masuala ya jinsia na mazingira.

### 2. HATUA YA UTEKELEZAJI WA KILA LENGU MKAKATI

Kazi zilizotekelezwa na TMDA katika kipindi cha mwaka 2020/21 kwa mujibu wa Mpango Kazi na Bajeti ni kama ilivyoainishwa katika vipengele 2.1 - 2.7.

### 2.1 KUHAKIKISHA USALAMA, UBORA NA UFANISI WA DAWA, VIFAA TIBA NA VITENDANISHI

Mamlaka ina jukumu la kulinda afya za wananchi dhidi ya athari ambazo zinaweza kujitokeza kutokana na matumizi ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Hii ni pamoja na kufanya usajili na ukaguzi wa bidhaa husika, kufuatilia madhara yatokanayo na dawa, vifaa tiba na vitendanishi pamoja na kufuatilia ubora na usalama wa bidhaa hizo katika soko. Katika kipindi cha mwaka 2020/21, chini ya lengo hili, Mamlaka ilitekeleza kazi zilizoaainishwa katika vipengele 2.1.1 – 2.1.11.

#### 2.1.1 Tathmini na Usajili wa bidhaa

##### 2.1.1.1 Tathmini na usajili wa dawa za binadamu.

Maombi 1,288 (mapya 693 na ya kuhuisha 595) yalipokelewa, vilevile kulikuwa na maombi 14 (mapya 11 na matatu (3) ya kuhuisha) yaliyobaki kufikia tarehe 30 Juni, 2020 na kufanya jumla ya maombi yote kuwa 1,302 (mapya 704 na ya kuhuisha 598). Kati ya maombi yote yaliyokuwepo maombi 1,218 (mapya 656 na ya kuhuisha 562) yalifanyiwa tathmini sawa na 94% ya maombi yote yaliyokuwepo. Katika kipindi hiki jumla ya maombi 1,111 (mapya 503 na ya kuhuisha 608) sawa na 91% yaliidhinishwa na kupatiwa usajili. Maombi yaliyoidhinishwa mwaka huu ni ongezeko la maombi manne (4) ikilinganishwa na maombi yaliyosajiliwa mwaka 2019/20. Mchanganuo wa tathmini na usajili wa dawa za binadamu umeainishwa kwenye Jedwali Na. 1(a).



Aidha, maombi mengine 2,166 (matangazo 393, mabadiliko 804 na hoja 969) yalipokelewa, vile vile kulikuwa na maombi mengine 45 (matangazo 2, mabadiliko 20 na hoja 23) yaliyobaki kufikia tarehe 30 Juni, 2020 hivyo kufanya maombi yote kuwa 2,211 (matangazo 395, mabadiliko 824 na hoja 992). Maombi 2,063 (matangazo 376, mabadiliko 748 na hoja 939) yalifanyiwa tathmini sawa na 93% ya maombi yote yaliyokuwepo. Maombi 1,124 (mabadiliko 746 na matangazo 378) yaliidhinishwa. Maombi mengine yaliyofanyiwa tathmini ni ongezo la maombi 215 (12%) ikilinganishwa na maombi mengine yaliyofanyiwa tathmini mwaka 2019/20. Mchanganuo wa tathmini ya maombi mengine umeainishwa kwenye **Jedwali Na. 1(b)**.

#### 2.1.1.2 Tathmini na usajili wa dawa za mifugo

Maombi 162 (mapya 119 na ya kuhuisha 43) yalipokelewa, vilevile kulikuwa na ombi moja (1) la kuhuisha lililobaki kufikia tarehe 30 Juni 2020 na hivyo kufanya jumla ya maombi yote kuwa 163 (mapya 119 na ya kuhuisha 44).

Kati ya maombi yote yaliyokuwepo maombi 148 (mapya 110 na ya kuhuisha 38) yalifanyiwa tathmini sawa na 91% ya maombi yote yaliyokuwepo ambapo maombi 83 (mapya 46 na ya Kuhuisha 37) yaliidhinishwa na kupatiwa usajili. Mchanganuo wa tathmini na usajili wa dawa za mifugo umeainishwa kwenye **Jedwali Na. 1(a)**.

Aidha, maombi mengine ya dawa za mifugo 108 (mabadiliko 23 na hoja 85) yalipokelewa, vilevile kulikuwa na maombi mawili (2) ya hoja yaliyobaki kufikia tarehe 30 Juni, 2020 na hivyo kufanya jumla ya maombi yote kuwa 110 (mabadiliko 23 na hoja 87).

Maombi 99 (mabadiliko 22 na hoja 77) yalifanyiwa tathmini ambapo maombi 15 ya mabadiliko yalidhinishwa na kupatiwa usajili. Mchanganuo wa tathmini ya maombi mengine umeainishwa kwenye **Jedwali Na. 1(b)**.

#### 2.1.1.3 Tathmini na usajili wa dawa za mitishamba

Maombi 27 (mapya 22 na ya kuhuisha 5) ya usajili wa mitishamba yalipokelewa. Maombi 25 (mapya 22 na ya kuisha 3) sawa na asilimia 92.6 yalifanyiwa tathmini ambapo maombi 4 (mapya 2 na Kuhuisha 2) yaliidhinishwa na kupatiwa Usajili kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 1 (a)**.

Maombi 2 ambayo hayakufanyiwa tathmini yalipokelewa mwisho wa mwaka na hivyo yatafanyiwa tathmini katika mwaka ujao wa fedha. Aidha, katika kipindi hiki kulikuwa na maombi 16 (mabadiliko 15 na hoja 1) yalipokelewa. Maombi 13 (mabadiliko 12 na hoja 1) yalifanyiwa tathmini kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 1(b)**.

#### 2.1.1.4 Tathmini na usajili wa vipukusi

Maombi 61 (mapya 55 na ya kuhuisha 6) ya usajili wa vipukusi yalipokelewa. Maombi 55 (mapya 51 na ya kuhuisha 4) sawa na asilimia 90.2 yalifanyiwa tathmini ambapo maombi 52 (mapya 42 na ya kuhuisha 10) yaliidhinishwa na kupatiwa usajili. Mchanganuo wa tathmini na usajili wa vipukusi umeainishwa kwenye **Jedwali Na. 1(a)**.

Vilevile, kulikuwa na maombi 14 (mabadiliko 11 na hoja 3) yalipokelewa ambapo maombi 13 (mabadiliko yalifanyiwa tathmini na ombi moja (1) la mabadiliko lilidhinishwa na kupatiwa usajili kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali Na. 1(b)**.

#### 2.1.1.5 Tathmini na usajili wa vifaa tiba

Jumla ya maombi 358 (mapya 284 na ya kuhuisha 74) ya usajili wa vifaa tiba yalipokelewa. Vilevile, kulikuwa na maombi 19 (mapya 15 na ya kuhuisha 4) yaliyobaki kufikia tarehe 30 Juni, 2020 hivyo kufanya jumla ya maombi yote kuwa 377 (mapya 299 na kuhuisha 78). Maombi 324 (mapya 250 na ya kuhuisha 74) yalifanyiwa tathmini ambayo ni sawa na asilimia 85.9. Kati ya hayo maombi 317 (mapya 249 na 68 huishwa) yalisajiliwa kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali 1(a)**.

Maombi 49 ambayo hayakufanyiwa tathmini yalipokelewa mwisho wa mwaka na hivyo yatafanyiwa tathmini katika mwaka ujao wa fedha. Vile vile maombi mengine 40 (matangazo 6, mabadiliko 22 na hoja 12) yalipokelewa.

Pia, kulikuwa na maombi 10 (mabadiliko 6 na hoja 4) yaliyobaki kufikia tarehe 30 Juni, 2020 hivyo kufanya jumla ya maombi yote kuwa 50 (matangazo 6, mabadiliko 28 na hoja 16). Maombi 48 (matangazo 6, mabadiliko 26 na hoja 16) sawa na asilimia 96 yalifanyiwa tathmini kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali 1(b)**.

#### 2.1.1.6 Tathmini na usajili wa vitendanishi

Maombi 159 mapya ya usajili wa vitendanishi yalipokelewa. Kulikuwa na maombi mapya 10 yaliyobaki kufikia tarehe 30 Juni, 2020 hivyo kufanya jumla ya maombi yote kuwa 169. Maombi 162 sawa na asilimia 96 yalifanyiwa tathmini ambapo maombi 124 yaliidhinishwa na kupatiwa usajili kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali 1(a)**.



Aidha, kulikuwa na maombi mengine 58 (mabadiliko 40, matangazo 5 na hoja 13) yaliyopokelewa. Kulikuwa na baki ya ombi moja (1) la hoja lililobaki kufikia tarehe 30 Juni, 2020 na hivyo kufanya jumla ya maombi yote kuwa 59 (mabadiliko 40, matangazo 5 na hoja 14). Maombi 57 (mabadiliko 38, matangazo 5 na hoja 14) sawa na asilimia 98.3 yalifanyiwa tathmini ambapo maombi 43 (matangazo 5 na mabadiliko 38) yalidhinishwa kama ilivyoainishwa kwenye **Jedwali 1(b)**.

#### 2.1.1.7 Utambuzi wa vifaa tiba na vitendanishi

Katika kipindi hiki, kulikuwa na maombi 3,206 ambapo maombi 2,521 yalikuwa ni ya vifaa tiba na 685 yalikuwa ni ya vitendanishi vyenye athari ndogo (low risk class A devices). Maombi yote yalifanyiwa tathmini na maombi 1,225 (Vifaa tiba 977 na vitendanishi 248) yaliidhinishwa. Sehemu kubwa ya maombi hayakuidhinishwa kwa sababu ya kukosa vigezo vya utambuzi ambapo mengi yalikuwa yanastahili kuombewa usajili.

#### 2.1.1.8 Tathmini ya maombi ya majaribio ya dawa

Jumla ya maombi 63 (mapya 18, mabadiliko 21 na hoja 24) ya majaribio ya dawa yalipokelewa na yote yalifanyiwa tathmini kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali Na.1(a) na Jedwali Na. 1(b).

Pia, jumla ya taarifa 93 za matukio makubwa ya kiafya (Serious Adverse Events-(SAE) yaliyotokea kwa washiriki wa majaribio ya dawa zilipokelewa na kufanyiwa tathmini.

Aidha, tathmini ilibaini kuwa matukio yaliyotokea hayakuhusiana na dawa zilizofanyiwa majaribio.

Vilevile taarifa 135 za Periodic safety update report (PSUR), 76 ya Periodic benefit-risk evaluation report (PBRER) na 20 za Risk Management Plan (RMP) zilipokelewa.

Taarifa 60 za PSUR na 20 za RMP zilifanyiwa tathmini na zote zilikidhi vigezo vya usalama wa dawa husika.

### JEDWALI 1(A): IDADI YA MAOMBI YA USAJILI WA BIDHAA ZA DAWA, VIFAA TIBA, VIPUKUSI, VITENDANISHI NA MAJARIBIO YA DAWA

Na.	Bidhaa	Maelezo	Baki ya Juni 2020	Pokelewa	Jumla	Tathminiwa	Idhinishwa	Kataliwa	Baki
1	Dawa za Binadamu	Mapya	11	693	704	656	503	5	48
		Huisha	3	595	598	562	608	0	36
		<b>Jumla Ndogo</b>	<b>14</b>	<b>1,288</b>	<b>1,302</b>	<b>1,218</b>	<b>1,111</b>	<b>5</b>	<b>84</b>
2	Dawa za Mifugo	Mapya	0	119	119	110	46	0	9
		Huisha	1	43	44	38	37	0	6
		<b>Jumla Ndogo</b>	<b>1</b>	<b>162</b>	<b>163</b>	<b>148</b>	<b>83</b>	<b>0</b>	<b>15</b>
3	Dawa za mitishamba	Mapya	0	22	22	22	2	0	0
		Huisha	0	5	5	3	2	0	2
		<b>Jumla Ndogo</b>	<b>0</b>	<b>27</b>	<b>27</b>	<b>25</b>	<b>4</b>	<b>0</b>	<b>2</b>
4	Vipukusi	Mapya	0	55	55	51	42	0	4
		Huisha	0	6	6	4	10	0	2
		<b>Jumla Ndogo</b>	<b>0</b>	<b>61</b>	<b>61</b>	<b>55</b>	<b>52</b>	<b>0</b>	<b>6</b>
5	Vifaa Tiba	Mapya	15	284	299	250	249	0	49
		Huisha	4	74	78	74	68	0	4
		<b>Jumla Ndogo</b>	<b>19</b>	<b>358</b>	<b>377</b>	<b>324</b>	<b>317</b>	<b>0</b>	<b>53</b>
6	Vitendanishi	Mapya	10	159	169	162	124	0	7
		<b>Jumla Ndogo</b>	<b>10</b>	<b>159</b>	<b>169</b>	<b>162</b>	<b>124</b>	<b>0</b>	<b>7</b>
7	Majaribio ya dawa	Mapya	0	18	18	18	11	0	0
		<b>Jumla Ndogo</b>	<b>0</b>	<b>18</b>	<b>18</b>	<b>18</b>	<b>11</b>	<b>0</b>	<b>0</b>
<b>JUMLA KUU</b>			<b>44</b>	<b>2,068</b>	<b>2,112</b>	<b>1,945</b>	<b>1,691</b>	<b>5</b>	<b>160</b>



Kwa mujibu wa Jedwali Na. 1 (a), jumla ya maombi 1,945 ya usajili wa dawa, vifaa tiba, vipukusi, vitendanishi na majaribio ya dawa yalifanyiwa tathmini ambapo maombi 1,691 yaliidhinishwa na bidhaa husika kusajiliwa.

Maombi yaliyotathminiwa katika kipindi hiki ni pungufu ya maombi 87(4%) ikilinganishwa na maombi 2,032 yaliyotathminiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2019/20. Upungufu huo

umetokana na kupungua kwa maombi ya usajili wa vipukusi ukilinganisha na mwaka uliopita kutokana na kuathirika kwa biashara duniani kwa sababu ya wimbi la kwanza la UVIKO-19. Katika kuendelea kuboresha udhibiti wa vifaa tiba na vitendanishi Mamlaka imetoa mafunzo kwa watathmini wapya kumi na nane (18) ili kuwajengea uwezo wa kufanya tathmini ya maombi ya usajili na kufanya ukaguzi wa vifaa tiba na vitendanishi.

## JEDWALI 1(B): MCHANGANUO WA MAOMBI MENGINE YANAYOHUSU USAJILI WA BIDHAA

Bidhaa	Maelezo	Baki ya Juni 2020	Pokelewa	Jumla	Tathminiwa	Idhinishwa	Kataliwa	Baki
Dawa za Binadamu	Matangazo	2	393	395	376	378	0	19
	Mabadiliko	20	804	824	748	746	0	76
	Hoja	23	969	992	939	NA	NA	53
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>45</b>	<b>2,166</b>	<b>2,211</b>	<b>2,063</b>	<b>1,124</b>	<b>0</b>	<b>148</b>
Dawa za Mifugo	Mabadiliko	0	23	23	22	15	0	1
	Hoja	2	85	87	77	NA	NA	10
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>2</b>	<b>108</b>	<b>110</b>	<b>99</b>	<b>15</b>	<b>0</b>	<b>11</b>
Dawa za mitishamba	Mabadiliko	0	1	1	1	0	0	0
	Hoja	0	15	15	12	NA	0	3
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>0</b>	<b>16</b>	<b>16</b>	<b>13</b>	<b>0</b>	<b>0</b>	<b>3</b>
Vipukusi	Mabadiliko	0	11	11	10	12	0	1
	Hoja	0	3	3	3	NA	NA	0
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>0</b>	<b>14</b>	<b>14</b>	<b>13</b>	<b>12</b>	<b>0</b>	<b>1</b>
Vifaa Tiba	Matangazo	0	6	6	6	6	0	0
	Mabadiliko	6	22	28	26	16	0	2
	Hoja	4	12	16	16	0	0	0
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>10</b>	<b>40</b>	<b>50</b>	<b>48</b>	<b>22</b>	<b>0</b>	<b>2</b>
Vitendanishi	Matangazo	0	5	5	5	5	0	0
	Mabadiliko	0	40	40	38	38	0	2
	Hoja	1	13	14	14	0	0	0
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>1</b>	<b>58</b>	<b>59</b>	<b>57</b>	<b>43</b>	<b>0</b>	<b>2</b>
Majaribio ya dawa	Mabadiliko	0	21	21	21	20	1	0
	Hoja	0	24	24	24	24	0	0
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>0</b>	<b>45</b>	<b>45</b>	<b>45</b>	<b>44</b>	<b>1</b>	<b>0</b>
<b>Jumla Kuu</b>		<b>58</b>	<b>2,447</b>	<b>2,505</b>	<b>2,338</b>	<b>1,260</b>	<b>1</b>	<b>167</b>

### **N/A: Not applicable**

Kwa mujibu wa Jedwali Na. 1 (b), jumla ya maombi 2,505 ya matangazo, majibu ya hoja na mabadiliko ya usajili wa bidhaa yalifanyiwa tathmini ambapo hadi kufikia June 2021 jumla ya maombi 1,260 yaliidhinishwa ikilinganishwa na maombi 1,283 yaliyoidhinishwa mwaka uliopita.

### **2.1.2 Usajili wa maeneo na utoaji wa vibali vya biashara ya dawa, vifaa tiba na bidhaa nyongeza**

Mfumo wa usajili wa maeneo ya biashara za bidhaa za dawa, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa

nyongeza husaidia kuhakikisha kuwa maeneo husika yanakidhi vigezo ili kutoathiri usalama, ubora na ufanisi wa bidhaa tajwa.

**Jedwali Na. 2** linaonesha mchanganuo wa usajili wa maeneo ya biashara.

## JEDWALI NA. 2: MAOMBI YA USAJILI WA MAENEO NA UTOAJI WA VIBALI VYA BIASHARA YA DAWA, VIFAA TIBA NA BIDHAA NYONGEZA

Aina ya jengo		Baki 2019/20	Yaliyopokelewa		Jumla	Yaliyotathmini wa	Yaliyosajiliwa	Vibali vilivyotolewa	Kataliwa/Hoja	% yaliyokidhi vigezo
			Mapya	Huisha						
Dawa	Duka la dawa la jumla (Binadamu)	2	37	107	146	146	134	134	12	92
	Duka la jumla la dawa (Mifugo)	1	10	49	60	60	60	60	0	100
	Maghala	0	14	30	44	42	39	39	3	93
	Maduka ya rejareja (mifugo)	2	2	0	4	2	2	2	0	100
	Magari ya kubebea dawa	0	23	41	64	64	64	64	0	100
<b>Jumla ndogo</b>		<b>5</b>	<b>86</b>	<b>227</b>	<b>318</b>	<b>314</b>	<b>299</b>	<b>299</b>	<b>15</b>	<b>95</b>
Vifaa tiba	Viwanda	1	2	7	10	10	7	7	3	70
	Vikubwa	2	7	0	9	9	5	5	0	56
	Kati	2	14	0	16	14	12	12	1	86
	Vidogo	2	14	0	16	14	12	12	1	86
<b>Jumla ndogo</b>		<b>5</b>	<b>23</b>	<b>7</b>	<b>35</b>	<b>33</b>	<b>24</b>	<b>24</b>	<b>4</b>	<b>73</b>
Vipukusi	Maduka ya Jumla	4	139	142	285	285	268	268	9	94
	Maduka ya rejareja	4	14	11	29	27	26	26	1	96
	Maghala	0	7	1	8	8	8	8	0	100
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>8</b>	<b>160</b>	<b>154</b>	<b>322</b>	<b>320</b>	<b>302</b>	<b>302</b>	<b>10</b>	<b>94</b>
	Viwanda	0	0	2	2	2	2	2	0	100
Vipukusi	Kati	0	0	2	2	2	2	2	0	100
	Vidogo	0	0	2	2	2	2	2	0	100
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>0</b>	<b>0</b>	<b>4</b>	<b>4</b>	<b>4</b>	<b>4</b>	<b>4</b>	<b>0</b>	<b>100</b>
<b>JUMLA KUU</b>		<b>18</b>	<b>269</b>	<b>392</b>	<b>679</b>	<b>671</b>	<b>629</b>	<b>629</b>	<b>29</b>	<b>94</b>

Jedwali Na. 2 linaonesha maombi 671 ya usajili wa maeneo ya biashara, yalishughulikiwa ambapo maombi 629 (94%) yaliidhinishwa kusajiliwa na kupewa vibali vya biashara.

Idadi ya maeneo yaliyosajiliwa katika kipindi hiki ni pungufu kwa maeneo 455 ikilinganishwa na maeneo 1,084 yaliyosajiliwa mwaka

uliopita. Sababu kubwa ya kushuka kwa maeneo yaliyosajiliwa imechangiwa na mwenendo wa biashara na uchumi kuwa sio mzuri kwa sababu ya uwepo wa UVIKO-19.

### 2.1.3 Ukaguzi wa maeneo ya biashara za dawa, vifaa tiba na vitendanishi nchini

Maeneo ya biashara za dawa, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyongeza hukaguliwa wakati wowote ili kuhakiki ubora wa majengo, usambazaji, uhifadhi na uuzaji ili kudhibiti ubora na usalama wa bidhaa hizo.

Maeneo hayo ni pamoja na famasi za dawa za binadamu na mifugo, hospitali, vituo vya afya, maghala, vifaa tiba na vitendanishi na magari ya kubebea bidhaa hizi. Mchanganuo wa maeneo yaliyokaguliwa umeainishwa katika **Jedwali Na.3.**



## JEDWALI NA. 3: UKAGUZI WA MAENEO YA BIASHARA ZA DAWA NA VIFAA TIBA NCHINI

Aina ya Biashara	Aina ya Jengo	Idadi	Yaliyokidhi vigezo	
			Idadi	%
Dawa	Maghala	88	71	81
	Duka la dawa/Famasi- binadamu (Jumla)	200	108	54
	Duka la dawa/famasi –binadamu (rejareja)	1,458	1,376	94
	Duka la dawa jumla (famasi) – Mifugo	427	359	84
	Duka la dawa muhimu (DLDM)- Binadamu	5,786	4,001	69
	Duka la dawa muhimu (DLDM)- mifugo	751	601	80
	Magari ya kubebea dawa	3	2	67
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>8,713</b>	<b>6,518</b>	<b>75</b>
	Hospitali	293	268	91
	Vituo vya afya	594	576	97
	Zahanati	588	515	88
	Maabara	457	331	72
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>1,932</b>	<b>1,690</b>	<b>87</b>
Vipukusi	Maghala	2	2	100
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>2</b>	<b>2</b>	<b>100</b>
	Maduka ya Jumla	127	96	76
	Maduka ya reja reja	58	48	83
Vifaa tiba	Maghala	14	10	71
	<b>Jumla ndogo</b>	<b>199</b>	<b>154</b>	<b>77</b>
<b>JUMLA KUU</b>		<b>10,846</b>	<b>8,364</b>	<b>77</b>

**Jedwali Na. 3** linaonesha kati ya maeneo 10,846 ya biashara za dawa, vifaa tiba na vipukusi yaliyokaguliwa, ukilinganisha na maeneo 8,283 kwa mwaka 2019/20. Aidha, maeneo 8,364 yalilikidhi vigezo ikilinganishwa maeneo 7,309 ya mwaka 2019/20. Ongezeko hili limechangiwa na kuimarika kwa shughuli za ukaguzi katika soko kufuatia Mamlaka kuongeza idadi ya wakaguzi na vitendea kazi.

Aidha katika kuendelea kuimarisha shughuli za ukaguzi wa dawa na vifaa tiba Mamlaka imetekeleza yafuatayo;

- a) Kuandaa mwongozo wa mafunzo kwa wakaguzi wa dawa na vifaa tiba (Inspectors Training Guide);
- b) Kutoa mafunzo ya wakaguzi wapya 55 wa dawa na vifaa tiba kutoka kanda zote za TMDA na ofisi ndogo ya makao makuu.
- c) Kutoa mafunzo kwa wakaguzi 6 wa vifaa tiba na vitendanishi wa Kanda ya Kaskazini na wakaguzi 34 wa Halmashauri ya Tanga; na
- d) Kufanya kikao cha wadau kwa ajili ya kupokea maoni kuhusiana na;
  - i. Kanuni za Good Storage and Distribution Practices (GSDP); na
  - ii. Kanuni za udhibiti wa bidhaa zitokanazo na tumbaku

### 2.1.4 Ukaguzi wa viwanda vya ndani na nje ya nchi

#### 2.1.4.1 Ukaguzi wa viwanda vya kutengeneza dawa ndani ya nchi.

Viwanda 9 kati ya 13 vilivyosajiliwa vilikaguliwa.

Jumla ya viwanda vipya 15 ambavyo ujenzi wake umefikia hatua mbalimbali na vinatarajiwa kuanza uzalishaji hivi karibuni. Viwanda hivi vimekuwa vikifanyiwa ukaguzi elekezi ili kuhakikisha kuwa vinakamilishwa kwa kuzingatia matakwa ya utengenezaji bora wa dawa.

#### 2.1.4.2 Ukaguzi wa viwanda vya kutengeneza vifaa tiba na gesi tiba ndani ya nchi.

Viwanda vyote 15 vilivyosajiliwa vilikaguliwa. Aidha, viwanda vipya 11 ambavyo ujenzi wake umefikia hatua mbalimbali na vinatarajiwa kuanza uzalishaji hivi karibuni. Viwanda hivi vimekuwa vikifanyiwa ukaguzi elekezi ili kuhakikisha kuwa vinakamilishwa kwa kuzingatia matakwa ya utengenezaji bora wa dawa.

Aidha, viwanda 14 vya gesi tiba vilikaguliwa ambapo viwanda vilivyokutwa na mapungufu mbalimbali vilielekezwa kurekebisha mapungufu hayo. Ukaguzi hakiki utafanyika mwaka ujao wa fedha.

Mchanganuo wa matokeo ya ukaguzi wa viwanda vya ndani umeainishwa kwenye **Jedwali Na. 4**

**JEDWALI NA. 4: MCHANGANUO WA MATOKEO YA VIWANDA VYA VYA NDANI  
VINAVYOJIHUSISHA NA UTENGENEZAJI VIFAA TIBA NA VITENDANISHI**

Na.	Aina ya Kiwanda	Vilivyo kaguliwa	Vilivyokidhi vigezo	Visivyokidhi vigezo	Vilivyo na hoja
1.	Viwanda vya vifaa tiba vilivyosajiliwa	15	0	0	15
2.	Viwanda vipya vya vifaa tiba	11	N/A	N/A	N/A
3.	Viwanda vya gesi tiba	14	3	0	11
<b>JUMLA</b>		<b>40</b>	<b>3</b>	<b>0</b>	<b>26</b>

**N/A: Not applicable**

Katika kuongeza uwezo na weledi wa uzalishaji wa vifaa tiba vilivyo bora na salama, Mamlaka imetoa mafunzo kwa wataalamu 40 kutoka katika viwanda saba (7) vya kutengeneza vifaa tiba vilivyopo nchini.

**2.1.4.3 Ukaguzi wa viwanda vya kutengeneza vipukusi ndani ya nchi**

Mamlaka ilikagua viwanda vinne (4) vya vipukusi ambapo vyote vilikidhi vigezo vya uzalishaji ikilinganishwa na viwanda 74 vilivyokaguliwa mwaka 2019/20.

**2.1.4.4 Ukaguzi wa viwanda vya kutengeneza dawa nje ya nchi**

Jumla ya maombi 151 ya ukaguzi wa viwanda vya kutengeneza dawa vilivyopo nje ya nchi yalipokelewa. Aidha, mpaka Julai, 2019 kulikuwa na jumla ya maombi 1110 ambayo yalikuwa ni baki kutoka katika vipindi vya nyuma. Maombi hayo yalikuwa katika hatua mbali mbali katika mfumo, hivyo kufanya maombi yote ambayo hayajafanyiwa kazi kwa sababu ya janga la UVIKO - 19 mpaka tarehe 30 Juni 2021 kuwa 1261.

Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Mamlaka iliandaa mwongozo uitwao "Guidelines on Submission of Documentation for Establishment of Compliance to Good Manufacturing Practices through Desk Assessment, Temporary Waiver and Virtual Inspection of Good Manufacturing Practices of Medicines and Quality Audit of Medical Devices during Emergencies".

Kupitia mwongozo huu, viwanda vinagawanywa katika makundi matatu (3) ambayo ni viwanda vinavyokidhi kufanyiwa ukaguzi kwa njia ya tathmini ya nyaraka (Desk assessment); viwanda vinavyostahili msamaha wa

kukaguliwa (temporary waiver to GMP inspection); na vile vinavyohitaji kufanyiwa ukaguzi kwa njia ya mtandao (virtual GMP inspection).

Utekelzaji wa mwongozo umeanza katika mwaka huu wa fedha ambapo jumla ya maombi 522 (41.4%) yalifanyiwa kazi.

**2.1.4.5 Ukaguzi wa viwanda vya kutengeneza vifaa tiba nje ya nchi.**

Jumla ya maombi tisa (9) ya ukaguzi wa viwanda vya kutengeneza vifaa tiba na vitendanishi vilivyopo nje ya nchi yalipokelewa. Vile vile kulikuwa na maombi 27 yaliyobaki kufikia tarehe 30 Juni 2020 hivyo kufanya maombi yote kuwa 36. Maombi yote 36 yalifanyiwa tathmini kwa njia ya uhakiki wa nyaraka (desk review) ambapo viwanda 36 vilikuwa na hoja za kujibu. Pia maombi matano (5) ya majibu ya hoja yalifanyiwa tathmini ambapo viwanda vitano (5) bado vina hoja za kujibu. Utaratibu wa desk review unatumika kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO - 19 ambapo ulisababisha kusimama kwa safari za nje ya nchi zilizokuwa zinahusika na ukaguzi wa viwanda hivyo.



#### 2.1.4.6 Ukaguzi maalum wa maeneo ya biashara ya vifaa tiba na vitendanishi

Ukaguzi maalum kwa lengo la kufuatilia na kubaini bidhaa duni na bandia za vifaa tiba na vitendanishi katika soko ulifanyika. Katika ukaguzi huo jumla ya maeneo 130 yanayojishusisha na uuzaji na utumiaji wa vifaa tiba na vitendanishi yalihakaguliwa.

Ukaguzi ulibaini na kukamata vifaa tiba duni, visivyosajiliwa, pamoja na vifaa tiba vya serikali

vinavyouzwa katika maduka ya dawa na vituo vya afya binafsi.

Pia, Mamlaka ilifanya ukaguzi maalum kwa wazalishaji, wasambazaji na watumiaji wa gesi tiba kwa lengo la kudhibiti ubora wa bidhaa hizo ambapo jumla ya maeneo 45 yaliyopo katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Musoma, Simiyu, Kagera na Geita yalihakaguliwa. Mchanganuo wa maeneo yaliyokaguliwa umeainishwa kwenye **Jedwali Na. 5.**

### JEDWALI NA. 5: MCHANGANUO WA MAENEO YA BIASHARA ZA VIFAA TIBA, VITENDANISHI NA GESI TIBA YALIYOKAGULIWA

Na.	Aina ya biashara	Maeneo yaliyokaguliwa
1.	Maduka ya vifaa tiba	66
2.	Maghala ya vifaa tiba	25
3.	Maabara	42
4.	Wazalishaji wa gesi tiba	14
5.	Wasambazaji wa gesi tiba	6
6.	Watumiaji wa gesi tiba	25
<b>Jumla</b>		<b>178</b>

Hatua mbalimbali zilichukuliwa na Mamlaka ikiwa ni pamoja na kuwafikisha katika vyombo vya dola wote waliokutwa na kuhusika moja kwa moja katika kusambaza au kuuza vifaa tiba au vitendanishi duni na vile vya serikali.

#### 2.1.4.7 Ukaguzi maalum wa maeneo ya biashara za dawa

Mamlaka ilifanya ukaguzi maalumu ambapo jumla ya majengo 894 (Famasi 334, maduka ya vifaa tiba 28, maghala ya dawa 21, maduka ya dawa za mifugo 15, Duka la Dawa Muhimu 329, vituo vya kutolea huduma za afya 29, maabara 28 na kiwanda cha dawa 1) yalihakaguliwa katika mikoa 19 nchini.

Katika ukaguzi huo dawa bandia aina tatu (3) zenye thamani ya TZS 857,000 zilikamatwa. Dawa hizo ni Alben Blue 2.5% (Albendazole 25%w/v) toleo namba 19394 iliyotengenezwa Novemba 2019 na kuisha muda wa matumizi Oktoba 2022 ambapo uchunguzi wa kimaabara ulionesha haina kiambata hai. Dawa nyingine ni Gentrison Cream 10g toleo namba GNTROX030 iliyotengenezwa Januari 2019 na kuisha muda wa matumizi Januari 2022, ambayo pia uchunguzi wa maabara imeonesha haina viambata hai vinavyotakiwa.

Dawa nyingine ni Benzathine Benzyl Penicillin Injection iliyoghushiwa lebo na kuandikwa benzallin (benzaithane Benzylthencillin Sodium Injection toleo namba 150947 iliyotengenezwa Januari 2019 na kumaliza muda wa matumizi Januari 2022. Uchunguzi umebaini kuwa kasha la nje linaonesha nguvu ya dawa ni 4 MU na kifungashio cha ndani kinaonesha ni 2 MU.

Aidha ukaguzi ulibaini na kukamata pia dawa mbalimbali za serikali zinazouzwa katika maduka ya dawa na vituo vya afya binafsi, dawa duni, dawa ambazo hazijasajiliwa, dawa zilizoisha muda wa matumizi ambazo zinazuzwa, vifaa tiba na vitendanishi duni na visivyo na usajili, vifaa tiba na vitendanishi vya serikali vilivyobainika kuuzwa katika maduka na vituo binafsi vya kutolea huduma za afya na maduka 53 yaliyokutwa yakiendeshwa bila vibali.

Hatua mbalimbali zilichukuliwa na Mamlaka ikiwa ni pamoja na kuwafikisha katika vyombo vya dola wote waliokutwa na kuhusika moja kwa moja katika kusambaza au kuuza dawa, vifaa tiba au vitendanishi bandia, vilivyoghushiwa tarehe za kuisha matumizi na vile vya serikali.

Jumla ya majalada 20 yalifunguliwa katika vituo vya polisi. Aidha, dawa duni, dawa zisizosajiliwa

na zilizoisha muda wa matumizi ziliteteketwa kwa mujibu wa sheria. Pia jumla ya TZS 86,388,695.5 zilikusanywa kama tozo (25% ya thamani ya bidhaa kama gharama ya kuteketeza na 2% kama tozo ya kukwepa kulipa gharama ya uingizaji nchini) kutoka kwa wafanyabiashara waliokutwa na makosa ambayo hayakuhitaji kuwafikisha mahakamani.

Mamlaka pia ilichukua sampuli za vipukusi mbalimbali aina ya vitakasa mikono (hand sanitizers) katika soko ambapo sampuli 195 zilichukuliwa katika soko na uchunguzi wa ubora wa bidhaa hizo ulifanyika katika maabara ya TMDA ambapo sampuli 124 zilikidhi vigezo vya ubora na 71 hazikukidhi vigezo vya ubora na kuelekezwa kuondolewa sokoni na watengenezaji wa hapa nchini kuelekezwa kurekebisha vigezo vya ubora vilivyoonekana kutokidhi.

#### 2.1.4.8 Ukaguzi vituo vya majaribio ya dawa

Katika kipindi hiki, Mamlaka ilifanya ukaguzi wa vituo vya majaribio ya dawa na chanjo ili kuhakiki kama yanakidhi vigezo vya kanuni za udhibiti wa majaribio ya dawa pamoja na matakwa ya Good

Clinical Practices (GCP). Jumla ya majaribio 23 yaliyopo katika vituo 7 vya majaribio ya dawa yalikaguliwa.

Majaribio hayo yanafanyika katika mkoa wa Mbeya (6), Pwani (5), Kilimanjaro (5), Mwanza (3) na Dar es Salaam (4). Vituo vyote vilivyokaguliwa vilikuwa na mapungufu madogo madogo ambapo watafiti wakuu walielekezwa kurekebisha mapungufu hayo na kuwasilisha taarifa TMDA.

#### 2.1.5 Udhibiti wa uingizaji nchini na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi

Katika kipindi husika, Mamlaka ilipokea maombi 13,003 ya vibali vya kuingiza nchini bidhaa zinazodhibitiwa na Mamlaka ambapo maombi 11,901 yaliidhinishwa. Aidha, kulikuwa na maombi 1,467 ya kusafirisha bidhaa husika nje ya nchi ambapo maombi 1,358 yaliidhinishwa.

Vilevile vibali 10,211 vya kuingiza bidhaa nchini na vibali 1,340 vya kusafirisha bidhaa nje ya nchi vilikaguliwa katika vituo mbalimbali vya forodha. Mchanganuo maombi yaliyopokelewa, vibali vilivyotelwa na vilivyokaguliwa umeanishwa katika **Jedwali Na.6.**

### JEDWALI NA. 6: MAOMBI YA VIBALI VYA KUINGIZA NCHINI NA KUSAFIRISHA BIDHA NJE YA NCHI

Na	Aina ya bidhaa	Yaliyopokelewa		Vibali vilivyotolewa		Vibali vilivyokaguliwa katika vituo vya forodha	
		Kuingia	Kutoka	Kuingia	Kutoka	Kuingia	Kutoka
1	Dawa	5,385	248	4,993	201	4,611	95
2	Malighafi - Dawa	635	-	598	-	401	-
3	Vifaa tiba na vitendanishi	6,982	1,219	6,310	1,157	5,199	1,245
	<b>Jumla</b>	<b>13,003</b>	<b>1,467</b>	<b>11,901</b>	<b>1,358</b>	<b>10,211</b>	<b>1,340</b>

Kwa kuzingatia **Jedwali Na. 6**, idadi ya vibali vilivyokaguliwa katika vituo vya forodha imeongezeka kwa 23% kutoka vibali 9,411 mwaka 2019/20 mpaka 11,551 mwaka 2020/21.

## 2.1.6 Ufuatiliaji wa ubora wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwenye soko (PMS)

### 2.1.6.1 Ufuatiliaji wa ubora wa dawa

Mamlaka iliandaa mipango miwili ya ufuatiliaji wa ubora wa dawa (PMS) ambapo mpango mmoja ulikuwa wa kufuatilia dawa za kutibu ugonjwa wa Malaria, Kifua kikuu na Kufubaza Virusi vya Ukimwi chini ya ufadhili wa Mfuko wa Dunia wa Hisani (Global Fund - GF) na mpango mwingine ulikuwa wa ufuatiliaji wa ubora wa dawa mbalimbali wa mwaka 2020 – 2023 kwa kutumia fedha za ndani. .

Jumla ya sampuli 342 zilikusanywa chini ya GF ambapo sampuli 159 zilikuwa za dawa Malaria, 80 Kifua kikuu na 103 Kufubaza Virusi vya Ukimwi katika mikoa 10 ambayo ni Kilimanjaro, Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma, Mwanza, Geita, Kagera, Mtwara na Mbeya.

Sampuli zote zilifanyiwa tathmini ya taarifa za lebo (product information review) ambapo sampuli 182 (53.2%) kati ya sampuli 342 hazikukidhi vigezo vya taarifa za lebo. Uchunguzi wa kimaabara kuhusu ubora wa dawa ambazo hazikukidhi vigezo vya taarifa za lebo unaendelea kufanyika ambapo hatua stahiki zitachukuliwa kutegemeana na matokeo ya uchunguzi.

Baadhi ya mapungufu yaliyobainishwa ni pamoja na kutokidhi matakwa ya maelekezo ya utunzaji wa dawa, lebo na karatasi ya maelekezo kwa mtumiaji kutokuwa na jina, anuani ya mtengenezaji na kutozingatia masharti ya lugha. Hata hivyo, sampuli zote zilifaulu uchunguzi wa kimaabara

Vile vile, katika Mpango wa mwaka 2020 - 2023 wa PMS, jumla ya sampuli 437 (ikiwa 343 za binadamu na 94 za mifugo) za aina ya Metronidazole, Metformin, Azithromycin, Telmisartan+ Hydrochlorothiazide, Levamisole, Sulfadiazin + Trimethoprimeza za awamu ya I na II kwa mwaka 2020/2021 zilikusanywa, kufanyiwa tathmini ya lebo (Product Information Review -PIR) na kuwasilishwa maabara kwa ajili ya uchunguzi ambapo matokeo ya uchunguzi yatawasilishwa katika ripoti ya robo ya kwanza ya mwaka 2021/22

Sampuli 437 (343 dawa za binadamu na 94 dawa za mifugo) zilifanyiwa tathmini ya taarifa za lebo (product information review) ambapo sampuli 296 (68%) kati ya sampuli 437 zilizokusanywa zilifeli katika tathmini hiyo. Kati ya sampuli ambazo hazikidhi vigezo vya taarifa za lebo, sampuli 233 (79%) zilikuwa za dawa za binadamu na sampuli 63 (21.3%) zilikuwa za dawa za mifugo.

### 2.1.6.2 Ufuatiliaji wa ubora wa vifaa tiba na vitendanishi

Jumla ya matoleo 668 ya bidhaa za vifaa tiba na vitendanishi yalipokelewa na kuwasilishwa maabara kwa ajili ya uchunguzi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa kuchunguza toleo kwa toleo (Pre distribution Lot to Lot Testing Programme). Kati ya matoleo 668, matoleo 666 yalifaulu, 13 bado yanaendelea na uchunguzi na matoleo 2 ya bidhaa aina ya kondom hayakukidhi vigezo. Mchanganuo wa aina na idadi za vifaa tiba na vitendanishi vilivyofanyiwa uchunguzi ni kama ilivyoainishwa hapa chini katika **Jedwali Na. 7.**



**Uchunguzi wa kimaabara kuhusu ubora wa dawa ambazo hazikukidhi vigezo vya taarifa za lebo unaendelea kufanyika ambapo hatua stahiki zitachukuliwa kutegemeana na matokeo ya uchunguzi.**

## JEDWALI NA. 7: MCHANGANUO WA MATOLEO YALIYUCHUNGUZWA (LOT TO LOT TESTING)

Na	Aina ya bidhaa	yaliyopo kelewa	yaliyochunguzwa	Yaliyokidhi Vigezo	Yasiyokidhi Vigezo
1.	Barakoa aina ya (Surgical Face Masks)	31	31	31	0
2.	Barakoa za kitambaa	3	3	3	0
3.	Barakoa aina ya KN95	3	3	3	0
4.	Glavu za uchunguzi (Examination Gloves)	14	14	14	0
5.	Kondom za kike	8	8	8	0
6.	Kondom za kiume	472	472	470	2
7.	Vipimo vya malaria (mRDT)	53	53	53	0
8.	Vipimo vya virusi vya UKIMWI (HIV Test)	75	75	75	0
9.	Vipimo vya virusi vya UKIMWI na kaswende (SD Bioline HIV/Syphilis Duo)	6	6	6	0
10.	Vipimo vya COVID-19 (nCov 19 Test)	3	3	3	0
<b>Jumla</b>		<b>668</b>	<b>668</b>	<b>666</b>	<b>2</b>

Aidha, Mamlaka ilitekeleza mpango wa ufuatiliaji wa ubora wa vitendanishi vya kupima Malaria (mRDTs) uliofadhiliwa na Mfuko wa Hisani wa Dunia (Global Fund) ambapo jumla ya matoleo 326 (81.5%) kati ya matoleo 400 ya sampuli za kupima Malaria (mRDTs) zilizopangwa yalikusanywa kutoka Bohari za Dawa, Hospitali, Vituo vya Afya, Zahanati na Maduka ya Dawa kutoka mikoa kumi (10) ya Tanzania Bara. Matokeo ya Tathmini ya lebo pamoja na uchunguzi wa kimaabara yalibainisha kuwa sampuli zote 326 (100%) zilifaulu tathmini hiyo na pia zilifaulu vipimo vya kuhakiki ubora na ufanisi.

Pia, katika kipindi husika Mamlaka ilitekeleza mpango wa ufuatiliaji wa ubora, usalama na ufanisi wa vifaa tiba na vitendanishi wa mwaka 2020-2023 kwa kukusanya jumla ya sampuli 284 za aina mbalimbali za vifaa tiba na vitendanishi ambazo zilikusanywa katika mikoa ya Lindi, Mara, Arusha, Dar es Salaam, Katavi, Tanga na Singida. Sampuli zote 284 zilifanyiwa tathmini ya taarifa kwenye vifungashio (PIR) ambapo Sampuli 254 zilifaulu na sampuli 30 hazijakidhi vigezo vya taarifa za kwenye lebo. Uchunguzi wa kimaabara wa sampuli zote utakamilika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22. Mchanganuo wa ukusanyaji wa sampuli umeandishwa kwenye **Jedwali Na. 8.**

## JEDWALI NA. 8: MCHANGANUO WA SAMPULI ZA VIFAA TIBA NA VITENDANISHI ZILIZOKUSANYWA

Na.	Aina ya bidhaa	Idadi ya sampuli zilizokusanywa	Zilizofaulu tathmini ya taarifa (PIR)	Zisizofaulu tathmini ya taarifa (PIR)	Sampuli zinazoendelea kufanyiwa uchunguzi wa maabara
1	Surgical Gloves	25	23	2	25
2	Kondom za Kiume	46	30	16	46
3	Cotton Wool	51	50	1	51
4	Surgical Sutures	40	33	7	40
5	Surgical Blades	25	21	4	25
6	mRDTs	51	51	0	51
7	HIV Test	46	46	0	46
<b>Jumla</b>		<b>284</b>	<b>254</b>	<b>30</b>	<b>284</b>



Vile vile Mamlaka iliandaa mpango wa miaka mitatu wa ufuatiliaji wa ubora, usalama na ufanisi wa vifaa tiba na vitendanishi wa mwaka (2020/21-2022/23) pamoja na andiko la “Quality of Medical Devices and In vitro Diagnostics in Tanzania “A national Post Marketing Surveillance” juu ya utekelezaji wa mpango wa miaka mitatu (2017/18 – 2019/20) wa ufuatiliaji ubora na ufanisi wa vifaa tiba na vitendanishi.

## **2.1.7 Ufuatiliaji wa usalama na matukio yanayohusiana na matumizi ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi**

### **2.1.7.1 Ufuatiliaji wa usalama na matukio yanayohusiana na matumizi ya dawa**

Jumla ya taarifa 6,713 za madhara yaliyohisiwa kusababishwa na matumizi ya dawa mbalimbali (Adverse Drug Reactions) zilipokelewa. Taarifa zote zilifanyiwa tathmini na kuingizwa kwenye kanzidata ya Vigiflow. Hakuna madhara yaliyohitaji kuchukuliwa hatua zaidi za kiudhibiti kwa kuwa madhara yote yaliyoripotiwa ni madhara yanayofahamika na tayari yalisharipotiwa katika kazi za nyuma za kisayansi ikiwa ni pamoja na kuwekwa katika taarifa za vifungashio vya dawa. Aidha, uchunguzi wa sampuli za dawa aina ya “Bupivacaine” zilizoripotiwa kuleta madhara kutoka mkoa wa Mbeya unaendelea kufanyika kabla ya kuchukua hatua stahiki.

Kazi ya ukusanyaji wa taarifa za usalama wa dawa (CEM) ya UKIMWI iitwayo Dolutegravir (DTG) ilifanyika katika vituo 28 vilivyochaguliwa. Vituo hivyo vipo katika mikoa 11 ya Dar es salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma, Iringa, Songwe, Arusha, Tanga, Mwanza, Geita na Shinyanga vilitembelewa ili kuangalia hatua iliyofikiwa katika ukusanyaji wa taarifa za usalama wa dawa ya UKIMWI aina ya Dolutegravir ambapo jumla ya wagonjwa 4,442 wanaotumia dawa hiyo wanafuatiliwa katika mikoa yote iliyochaguliwa. Katika kutekeleza kazi hiyo jumla ya wataalam 285 walipatiwa mafunzo ya ukusanyaji wa taarifa husika.

### **2.1.7.2 Ufuatiliaji wa usalama na matukio yanayohusiana na vifaa tiba na vitendanishi**

Mamlaka ilitekeleza kazi ya uhamasishaji watumishi wa afya juu ya utoaji taarifa dhidi ya madhara na matukio yatokanayo na matumizi ya vifaa tiba na vitendanishi katika mikoa ya Kilimanjaro, Morogoro, Tabora, Lindi, Tanga,

Mwanza na Geita ambapo jumla ya watumishi 1,055 walihamasishwa.

Aidha, jumla ya taarifa 165 za matukio yatokanayo na matumizi ya vifaa tiba na vitendanishi duni zilipokelewa na kufanyiwa tathmini na hatua mbali mbali zilichukuliwa ikiwemo uondoaji wa bidhaa hizo katika soko na kusitisha matumizi ya vifaa mathalan vifaa tiba vikubwa.

Vilevile, Mamlaka ilifanya mapitio ya taratibu za ufuatiliaji wa usalama wa vifaa tiba na vitendanishi katika soko ambapo mwongozo uliokuwepo umefanyiwa mapitio kwa kuongeza taratibu za tathmini za madhara na matukio yatokanayo na matumizi ya vifaa tiba na vitendanishi pamoja na hatua za kuchukua.

## **2.1.8 Uwianisho wa taratibu za udhibiti wa Dawa wa Jumuiya za Kikanda**

### **2.1.8.1 Tathmini ya pamoja na usajili wa dawa za binadamu katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)**

Jumla ya maombi 48 yalipokelewa yakiwemo mapya 25 na majibu ya hoja 23). Vilevile, kulikuwa na maombi 13 (mapya 4 na hoja 9) yaliyobaki kufikia tarehe 30 Juni 2020 hivyo kufanya jumla ya maombi yote kuwa 61 (mapya 29 na hoja 32).

Kati ya maombi yote yaliyokuwepo jumla ya maombi 45 yalifanyiwa tathmini ambapo maombi kumi (10) yalipendekezwa kupewa usajili. Mchanganuo wa tathmini umeainishwa kwenye **Jedwali Na. 9**

### **2.1.8.2 Tathmini ya pamoja na usajili wa dawa za Binadamu chini ya ushirikiano wa nchi za SADC (ZAZIBONA)**

Jumla ya maombi 18 ya usajili wa dawa yalipokelewa yakiwemo 12 mapya na 6 majibu ya hoja. Maombi 12 yalifanyiwa tathmini ambapo maombi tisa (9) yalipendekezwa kupewa usajili. Mchanganuo wa tathmini umeainishwa kwenye **Jedwali Na. 9**

### **2.1.8.3 Tathmini ya maombi ya usajili wa dawa za binadamu chini ya ushirikiano na Shirika la Afya Duniani (WHO) - Collaborative - Registration Procedure (CRP)**

Maombi 6 (5 dawa na 1 vitendanishi) yalipokelewa ambapo maombi 4 dawa na 1 vitendanishi yamefanyiwa tathmini na kusajiliwa. Mchanganuo wa tathmini umeainishwa kwenye **Jedwali Na. 9**

## JEDWALI NA. 9: TATHMINI NA USAJILI WA DAWA ZA BINADAMU JUMUIYA ZA KIKANDA

Aina ya Usajili	Aina	Baki ya Juni 30, 2020	Pokelewa	Jumla	Tathminiwa	Baki	Pendekezwa	Sajiliwa
EAC	Mapya	4	25	29	23	6	0	0
	Hoja	9	23	32	22	10	10	10
<b>Jumla ndogo</b>		<b>13</b>	<b>48</b>	<b>61</b>	<b>45</b>	<b>16</b>	<b>10</b>	<b>10</b>
SADC (ZAZIBONA)	Mapya	0	12	12	12	0	9	7
	Hoja	0	6	6	5	1	0	0
<b>Jumla ndogo</b>		<b>0</b>	<b>18</b>	<b>18</b>	<b>17</b>	<b>1</b>	<b>9</b>	<b>7</b>
WHO-CRP	Mapya -dawa	0	5	5	4	1	4	4
	Hoja-dawa	0	0	0	0	0	0	0
	Mapya-vitendanishi	0	1	1	1	0	0	1
<b>Jumla ndogo</b>		<b>0</b>	<b>6</b>	<b>6</b>	<b>5</b>	<b>1</b>	<b>4</b>	<b>5</b>
<b>JUMLA KUU</b>		<b>13</b>	<b>72</b>	<b>85</b>	<b>67</b>	<b>18</b>	<b>23</b>	<b>22</b>

### 2.1.8.4 Ukaguzi wa viwanda vya dawa za binadamu Kikanda

Kiwanda kimoja (1) cha Mylan, Zambia kilifanyiwa ukaguzi wa pamoja kwa njia ya mtandao (virtual inspection) chini ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Africa (SADC) ambapo hoja mbalimbali zilitolewa na majibu ya hoja hizo (CAPA) yamepokelewa na kimekidhi matakwa ya utengenezaji sahihi wa dawa.

### 2.1.9 Utekelezaji wa Miradi ya "PAVIA", "PROFORMA" na "ASCEND"

Mamlaka ilitekeleza miradi ya PAVIA, PROFORMA na ASCEND kupitia ufadhili wa EDCTP ambapo kazi zifuatazo zilitekelezwa: -

- Mpango wa Taifa wa Ufuatiliaji wa Usalama wa Dawa (National Pharmacovigilance Roadmap) uliandaliwa na kuidhinishwa kwa ajili ya kutumika.
- Kuunganisha mifumo ya kielektroniki ya aDSM na ARRT inayotumika kutolea taarifa za madhara ya dawa za TB kutoka kwenye vituo vya afya ambapo taarifa hizo zinapokelewa na TMDA moja kwa moja;
- Kutoa mafunzo kwa watumishi 12 wa TMDA juu ya kufanya tathmini za taarifa za Periodic safety update report (PSUR), Periodic benefit-risk evaluation report (PBRER) na Risk management plan (RMP) ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya taarifa husika;
- Kuandaa andiko (abstract) lenye jina la "Increase in reporting of adverse drug reactions of anti-TB medication after implementation of the PAVIA programme in Tanzania" na andiko hilo limekubalika na litawasilishwa kwenye mkutano wa 52 wa

"Union World Conference on Lung health" utakaofanyika mwezi Oktoba 2021;

- Kutengeneza tovuti ya mradi wa ASCEND ambapo tovuti husika (<http://ascend.tmda.go.tz/ascend/>) pamoja na account za mitandao ya kijamii ambazo ni Instagram ASCENDEDCTP na twitter ASCEND-EDCTP;
- Kuboresha mfumo wa kielektroniki wa kutolea taarifa za matukio yatokanayo na matumizi ya dawa (SAEs) na kuwafundisha watumiaji namna ya kutumia mfumo huo;
- Kufuatilia na kupata kibali kutoka Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania cha kuendesha mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ya shahada ya uzamili ya Pharmacovigilance na Pharmacoepidemiology ambapo mafunzo hayo yataendeshwa na Chuo Kikuu cha Afya cha Muhimbili; na
- Kuandaa mpango wa ufuatiliaji na tathmini wa mradi wa ASCEND.

### 2.1.10 Utekelezaji wa bidhaa zisizokidhi viwango

Mamlaka huteketeza bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi ambazo hazikidhi vigezo vya ubora usalama na ufanisi ili kuepusha bidhaa husika zisitumiwe na walaji. Bidhaa zinazoteketezwa zinajumuisha zile zinazoombewa kibali (voluntary disposal) na wateja wenyewe kutokana na kuisha muda wa matumizi na zilizokamatwa katika kaguzi mbalimbali kwa sababu hazijasajiliwa, kuwa duni/bandia baada ya uchunguzi wa kimaabara au zinazokutwa kwenye maeneo ambayo hayajasajiliwa na TMDA. Uzito na thamani za bidhaa zilizoteketezwa kwa kipindi hiki umeainishwa katika **Jedwali Na. 10**.

## JEDWALI NA. 10: MCHANGANUO WA BIDHAA ZISIZO NA UBORA ZILIZOTEKETEZWA

Na.	Aina ya bidhaa	Mchanganuo			
		Vilivyotolewa taarifa		Vilivyokamatwa	
		Uzito (MT)	Thamani (TZS)	Uzito (MT)	Thamani (TZS)
1.	Dawa za binadamu	8,212.94	5,472,695,454.26	60.49	712,867,983.00
2.	Dawa za mifugo	0.25	1,400,000.00	0.40	17,723,852.00
3.	Vifaa tiba	6,491.61	2,981,072,590.02	1.54	17,978,200.00
4.	Vipukusi	-	-	0.01	1,405,500.00
<b>Jumla</b>		<b>14,704.80</b>	<b>8,455,168,044.28</b>	<b>62.44</b>	<b>749,975,535.00</b>

Kwa mujibu wa Jedwali Na. 10 hapo juu, jumla ya tani 14,704.80 za bidhaa zenye thamani ya takriban TZS 8,455,168,044.28/= zilizotekezwa kutokana na kutokidhi vigezo vya ubora na usalama hivyo kutofaa kwa matumizi ya binadamu.

### 2.2 KUBORESHA HUDUMA ZA MAABARA

Maabara za TMDA zinajukumu la kufanya uchunguzi wa sampuli za dawa, vifaa tiba, vitendanishi, vifungashio vya bidhaa hizo, malighafi zake pamoja na kufanya tafiti na mafunzo.

Jumla ya sampuli 3,322 za dawa, vifaa tiba, vitendanishi na vipukusi zilipokelewa, ambapo kati ya hizo sampuli 3,197 zilipokelewa katika Maabara ya Dar es salaam na 125 zilipokelewa katika Maabara ya Mwanza. Vilevile, kulikuwa na sampuli 591 ambayo ni baki kutoka mwaka wa fedha wa 2019/20 hivyo kufanya jumla ya sampuli kuwa 3,913. Sampuli 3,603 sawa na 92.1% zilifanyiwa uchunguzi katika maabara zote (Dar es Salaam 3,474 na Mwanza 129) ambapo jumla ya sampuli 3,179 (88.2%) zilifaulu.



Aidha sampuli 782 za dawa zilipokelewa na kufanyiwa kazi katika vituo vya maabara hamishika vilivyopo katika hospitali za mikoa, vituo vya forodha na Ofisi za Kanda. Mchanganuo wa sampuli za dawa, vifaa tiba, vitendanishi na vipukusi umeainishwa katika vipengele 2.2.1 – 2.2.6.

#### 2.2.1 Uchunguzi wa sampuli za dawa

Kulikuwa na jumla ya sampuli 2534 za dawa zilipaswa kuchunguzwa ambapo sampuli 2164 kati ya hizo zilipokelewa katika kipindi cha Julai 2020 - Juni 2021 na sampuli 370 ilikuwa ni baki ya mwaka wa fedha 2019/20. Sampuli 2,358 (90.4%) zilichunguzwa ambapo 2,322 (98.5%) zilifaulu kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 11(a) uchunguzi wa sampuli 176 zilizobakia utakamilika na taarifa yake itatolewa katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22.

## JEDWALI NA. 11 (A): UCHUNGUZI WA SAMPULI ZA DAWA

Chanzo cha sampuli	Baki (2019/20)	Pokelewa	Jumla	Chunguzwa	Baki	Faulu	% Faulu
<b>Maabara ya Dar es Salaam</b>							
Usajili – dawa za binadamu	0	11	11	6	5	1	16.67
Ukaguzi-dawa za binadamu	0	93	93	83	10	73	87.95
Wateja wa nje-binadamu	0	41	41	36	5	26	72.22
Uchunguzi wa awali	366	1,156	1,522	1,366	156	1,365	99.92
Ufuatiliaji katika soko (PMS)	0	790	790	790	0	781	98.86
Pharmacovigilance	0	1	1	1	0	1	100
<b>Jumla ndogo</b>	366	2,092	2,458	2,282	176	2,247	98.47
<b>Maabara ya Mwanza</b>							
Ukaguzi-binadamu	0	1	1	1	0	0	0
Ufuatiliaji katika soko (PMS)	4	71	75	75	0	75	100
<b>Jumla ndogo</b>	4	72	76	76	0	75	98.68
<b>JUMLA KUU</b>	370	2,164	2,534	2,358	176	2,322	98.51

Kwa mujibu wa Jedwali Na 11 (a) kiwango cha ufaulu wa 98.51% wa sampuli za dawa zilizochunguzwa katika maabara kinatoa hakikisho kwa watumiaji wa bidhaa hizo nchini. Aidha usajili wa sampuli 5 za dawa za binadamu ambazo hazikukidhi vigezo haukufanyika ambapo wahusika waliarifwa juu ya mapungufu na taratibu za ukamilishaji wa usajili.

### 2.2.2 Uchunguzi wa sampuli za vifaa tiba na vitendanishi

Katika kipindi husika Mamlaka ilipokea jumla ya sampuli 1,042 (vifaa tiba 596 na vitendanishi 446). Aidha, kulikuwa na baki ya sampuli 221 kutoka mwaka wa fedha 2019/20 na hivyo kufanya jumla ya sampuli kuwa 1,263. Sampuli 1,129 (89.39%) zilichunguzwa ambapo 760 (67.3%) zilifaulu kama

ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 11 (b). Uchunguzi wa sampuli 134 zilizobakia unaendelea na taarifa yake itatolewa katika robo ya kwanza ya mwaka 2021/22

### 2.2.3 Uchunguzi wa sampuli za vipukusi

Mamlaka ilipokea jumla ya sampuli 116 za vipukusi (Dar es Salaam 63 na Mwanza 53). Sampuli 116 (100.0%) zilichunguzwa ambapo 97 (83.6%) zilifaulu kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 11 (c)**

## JEDWALI NA. 11 (B) : UCHUNGUZI WA SAMPULI ZA VIFAA TIBA NA VITENDANISHI

Bidhaa	Chanzo cha Sampuli	Baki kutoka 2019/20	Pokelewa	Jumla	Chunguzwa	Baki	Faulu	% Faulu
Vifaa tiba	Ukaguzi	81	546	627	578	49	252	43.6
	Wateja wa nje	7	46	53	46	7	46	100
	Usajili	0	0	0	0	0	0	0
	PMS	119	4	123	63	60	34	54.8
	<b>Jumla ndogo</b>	207	596	803	687	116	332	48.3
Vitendanishi	Ukaguzi	0	114	114	111	3	97	87.4
	Wateja wa nje	1	5	6	4	2	4	100
	Usajili	0	3	3	3	0	3	100
	PMS	13	324	337	324	13	324	100
	<b>Jumla ndogo</b>	14	446	460	442	18	428	96.8
<b>JUMLA KUU</b>		<b>221</b>	<b>1042</b>	<b>1263</b>	<b>1129</b>	<b>134</b>	<b>760</b>	<b>67.3</b>

**Jedwali Na. 11 (b)** linaonesha kuwa kiwango cha ufaulu wa 67.4% wa vifaa tiba na vitendanishi vilivyoko katika soko ni salama na bora kwa watumiaji.

## JEDWALI NA. 11 (C): UCHUNGUZI WA SAMPULI ZA VIPUKUSI

Chanzo cha sampuli	Pokelewa	Jumla	Chunguzwa	Faulu	% Faulu
Ukaguzi	31	31	31	27	87.1
Wateja wa nje	19	19	19	15	78.9
Usajili	13	13	13	7	53.8
<b>Jumla ndogo</b>	<b>63</b>	<b>63</b>	<b>63</b>	<b>49</b>	<b>77.7</b>
Usajili	1	1	1	0	0
Ukaguzi	7	7	7	7	100
Ufatiliaji wa bidhaa sokoni (PMS)	45	45	45	41	91.1
<b>Jumla ndogo</b>	<b>53</b>	<b>53</b>	<b>53</b>	<b>48</b>	<b>90.5</b>
<b>JUMLA KUU</b>	<b>116</b>	<b>116</b>	<b>116</b>	<b>97</b>	<b>83.6</b>

### 2.2.4 Uchunguzi wa awali wa dawa katika maabara hamishika (minilab kits)

Jumla ya maabara hamishika 19 zimeweza kuchunguza jumla ya sampuli 782 kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2021 kulinganisha na sampuli 677 mwaka 2019/2020, sampuli zote zilikidhi viwango vya ubora.

Dawa za aina 22 na zimegawanyika kwa makundi ya Dawa za kufubaza makali ya Ukimwi, Dawa za kutibu Malaria, Dawa za kutibu Kifua Kikuu, Dawa za kutibu Minyoo, dawa za kutibu shinikizo la damu, dawa za Viuasumu, dawa za kutibu athma/Mzio, Dawa za kupunguza Maumivu. Vituo hivi vimechunguza kati ya sampuli 0 – 157, wastani wa sampuli 20 kwa kituo kwa mwaka wa fedha (Julai 2020 - Juni 2021) kama inavyoonekana katika **Jedwali Na 12**

Aidha, Mamlaka katika zoezi la kuangalia umahiri wa upimaji “Proficiency Testing” (PT), iliandaa na kutuma sampuli husika katika vituo 22 vyenye maabara hamishika. Majibu ya PT kutoka vituo kumi na nne (14) tu yalipokelewa kati ya vituo 22 vilivyoshirikishwa ambavyo ni Geita RRH, Manyara RRH, TMDA Kanda ya Kaskazini, Mawenzi RRH, Namanga POE, Mutukula POE, Sirari POE, Mbeya RRH, Horohoro



POE, Tunduma OSBP, TMDA Kanda ya Magharibi, Tanga RRH, Ruvuma RRH na Sokoine (Lindi) RRH. Vituo nane (8) havikurudisha majibu kutokana na ugumu wa kufanya uchunguzi wa TB vituo hivyo ni pamoja na Kagera RRH, Mara RRH, Mtwara RRH, Rukwa RRH, Iringa RRH, TMDA Kanda ya Kati, Kigoma RRH na Katavi RRH. Kati ya vituo 14 vilivyorudisha majibu, vituo 8 vilifaulu. Kutokana na changamoto baadhi ya vituo kushindwa kupima dawa za TB, Mamlaka imepanga kuandaa mafunzo kwenye eneo hilo katika mwaka wa fedha 2021/22.



**Dawa za aina 22 na zimegawanyika kwa makundi ya Dawa za kufubaza makali ya Ukimwi, Dawa za kutibu Malaria, Dawa za kutibu Kifua Kikuu, Dawa za kutibu Minyoo, dawa za kutibu shinikizo la damu, dawa za Viuasumu, dawa za kutibu athma/Mzio, Dawa za kupunguza Maumivu.**

## JEDWALI NA. 12 : VITUO VYA MAABARA HAMISHIKA

Na.	KANDA	KITUO CHA MAABARA HAMISHIKA	IDADI YA SAMPULI ZILIZOCHUNGUZA
1.	Kanda ya Ziwa	1. Geita RRH	60
		2. Kagera RRH	91
		3. Mara RRH	5*
		4. Sirari - POE	2*
		<b>Jumla ndogo</b>	<b>158</b>
2.	Kanda ya Kaskazini	1. Manyara RRH	22
		2. Mawenzi RRH	46
		3. Namanga - POE	52
		4. TMDA - Arusha	157
		<b>Jumla ndogo</b>	<b>277</b>
3.	Kanda ya Mashariki	1. Bombo RRH	9*
		2. EZ - TMDA	45
		<b>Jumla ndogo</b>	<b>54</b>
4.	Kanda ya Kusini	1. Lindi RRH	4*
		2. Mtwara RRH	42
		3. Ruvuma RRH	20
		<b>Jumla ndogo</b>	<b>66</b>
5.	Kanda ya Nyanda za juu Kusini	1. Mbeya RRH	25
		2. Tunduma - OSBP	44
		3. Iringa RRH	80
		<b>Jumla ndogo</b>	<b>149</b>
6.	Kanda ya Magharibi	1. Tabora RRH	21
		2. Kigoma RRH	29
		3. Katavi RRH	28
		<b>Jumla ndogo</b>	<b>78</b>
		<b>Jumla Kuu</b>	<b>782</b>

**Ufunguo:** RRH: Regional Referral Hospital POE: Port of Entry

\*Vituo ambavyo vilichunguza idadi ndogo ya sampuli kwa sababu baadhi ya watendaji waliopewa mafunzo walihamishwa vituo vya kazi. Aidha, shehena chache huingizwa nchini kupitia kituo cha Forodha cha Sirari.

### 2.2.5 Utekelezaji wa mifumo ya ubora wa kazi (ISO/IEC17025 na WHO/GLP)

Katika kuhakikisha kuwa mifumo ya ubora wa kazi (ISO/IEC 17025 na WHO/GLP) ya maabara inaimarika, Mamlaka ilitekeleza kazi zifuatazo:-

- i. Kutekeleza matakwa ya kiwango cha ISO/IEC 17025:2017 kwa uchunguzi wa Vifaa Tiba na Vitendanishi, pamoja na Mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO/GPPQCL) wa Utambuzi wa Maabara (WHO Prequalification) kwa upande wa uchunguzi wa Dawa na Bidhaa nyongeza. Hii ilihakikisha ubora wa kazi za uchunguzi wa sampuli katika Maabara; na
- ii. Kufanya tathmini kuhusu huduma zitolewazo na maabara kwa wateja (Laboratory customer survey) ambapo tathmini iliyofanyika ilionyesha asilimia 84 ya wateja waliridhishwa na huduma za maabara.

### 2.2.6 Ugezi, Matengenezo na Ununuzi wa vifaa, Kemikali na Mahitaji mengine ya Maabara

Mamlaka imeweza kutekeleza kazi za ugezi, matengenezo ya vifaa vya maabara, ununuzi wa kemikali, vifaa na consumables kama ilivyopangwa katika mpango kazi na mpango wa manunuzi wa mwaka.

### 2.3 KUIMARISHA UTOAJI ELIMU KWA UMMA NA KUBORESHA HUDUMA KWA WATEJA

Mamlaka hutoa elimu kwa umma ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa sahihi juu ya kazi na majukumu ya TMDA, mahitaji ya Sheria sanjari na kujengewa uelewa wa taratibu za kuanzisha biashara ili kukidhi vigezo vya usalama na ubora wa bidhaa zinazodhibitiwa. Kazi zifuatazo zilitekelezwa ili kuelimisha umma.

#### 2.3.1 Elimu kwa umma

Elimu kwa umma husaidia kuongeza uelewa kwa watumiaji wa bidhaa zinazodhibitiwa na TMDA na wananchi kwa ujumla na hivyo kusaidia matumizi sahihi ya bidhaa pamoja na kuongeza utii wa sheria bila shuruti. Kazi za uelimishaji umma zilizotekelezwa ni kama zilizoorodheshwa katika **Jedwali Na. 13**.

## JEDWALI NA. 13: NJIA ZILIZOTUMIKA KUELIMISHA JAMII

Na	Kazi zilizopangwa	Idadi	Utekelezaji
1	Kutoa elimu kwa njia ya mihadhara (outreach campaigns)	283,160	Kutoa elimu kwa njia ya mihadhara kwa wananchi wanafunzi na waalimu wa shule za sekondari 102 pamoja na vikundi vya maendeleo katika wilaya za Mvomero, Babati, Nzega na Morogoro, Lindi, Mtwara, Rufiji, Kibiti, Tanga, Bagamoyo, Morogoro, Mvomero, Uyui, Kongwa, Tabora, Mkalama, Arumeru, Karatu, Monduli, Longido. Mwanza, Misungwi, Ukerewe, Magu, Kwimba, Sengerema, Nyamagana, Ilemela na Geita
2.	Maonesho na mikutano	7	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kushiriki katika maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Sabasaba, maonesho ya wakulima Nanenane na maonesho ya Biashara ya Afrika Mashariki jijini Mwanza, na mkutano wa Wafamasia pamoja na maadhimisho ya wiki ya magonjwa yasiambukizwa (NCDs), tukio la Temeke <i>Onestop</i> Jawabu na maonesho ya bidhaa za viwanda vya Tanzania</li> </ul>
3.	Vipindi na matangazo mafupi ya redio na runinga	20  10	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kuandaa, kuhariri na kurusha vipindi 14 vya TMDA na Jamii pamoja na matangazo mafupi ya uelimishaji kuhusu kazi na majukumu ya TMDA kupitia TV na Radio za kibiashara na kijamii.</li> <li>Kuandaa script za vipindi vya uelimishaji kwa njia ya redio ambapo vipindi 10 kuhusu kazi na majukumu ya TMDA viliandaliwa</li> </ul>
4.	Kuandaa vielelezo vya uelimishaji na vifaa vya kutangaza huduma za TMDA	8	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kuandaa na kuhariri jarida la TMDA toleo la Nane (8) na Tisa (9), jarida la usalama wa dawa toleo la nne (4) pamoja na uchapaji wa taarifa ya utafiti kuhusu utoaji huduma (SDS main report vol 1 &amp; 2)</li> <li>Kuandaa mwongozo wa mafunzo ya huduma kwa wateja (customer care training manual), mwongozo wa ufundishaji dhana ya utoaji huduma bora (Customer Care Training Guide) na mwongozo wa utoaji matangazo ya bidhaa kupitia vyombo vya habari .</li> </ul>
5.	Taarifa kwa umma na Matangazo	22	<ul style="list-style-type: none"> <li>Taarifa kwa umma na matangazo kuhusu kazi na majukumu ya TMDA na udhibiti wa bidhaa yalitolewa kwa wananchi na wadau mbalimbali kwa njia ya magazeti, kurasa za mitandao ya kijamii na tovuti ya TMDA</li> </ul>
6.	Tovuti na kurasa za TMDA kwenye mitandao ya jamii	5	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kuhuisha taarifa na matukio katika tovuti ya TMDA na kurasa za TMDA katika mitandao ya kijamii</li> </ul>
7.	Mikutano na waandishi wa habari	6	<ul style="list-style-type: none"> <li>Kuendesha vikikao kazi 2 kuhusu kazi na majukumu ya TMDA cha Waandishi na Wahariri kutoka vyombo mbalimbali vya habari katika mkoa ya Morogoro (Julai, 2020 na Arusha (Juni, 2021).</li> <li>Kufanya Mikutano miwili (2) na waandishi wa Habari kuhusu matokeo ya ukaguzi maalumu ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi uliuoendeshwa nchi nzima na kuanza kwa mradi wa ASCEND.</li> <li>Kuandaa ziara ya waandishi wa habari katika maabara za TMDA zilizopo Dar es salaam na Mwanza ambapo makala na habari mbalimbali za kuitangaza maabara ziliandaliwa na kurushwa kupitia vyombo vya habari</li> </ul>

### 2.3.2 Kuboresha huduma kwa wateja

Katika kuhakikisha kuwa utoaji wa huduma kwa wateja ni wa kiwango bora, Mamlaka ilitekeleza kazi zifuatazo:-

- i. Kuboresha namba ya wateja kupiga simu bila malipo (Toll Free) kwa kuandaa na kuweka jumbe mbalimbali zinazotumika kama miito na maelezo ya msaada kwa wateja wanaopiga simu;
- ii. Kuendesha mafunzo kuhusu dhana ya utoaji huduma bora kwa watumishi 32 wanaohudumia wateja katika madawati ya huduma kwa wateja pamoja na watumishi waliohamia TMDA;
- iii. Kuandaa mfumo wa kielektroniki wa kukusanya na kuchakata maoni ya wateja kupitia dodoso (customer exit interview questionnaire) ambapo madodoso 98 yaliyojazwa yalipokelewa na maoni yamefanyiwa kazi;
- iv. Kuhudumia wateja 12,558 kupitia madawati ya huduma kwa wateja na 267 kupitia maktaba iliyopo Ofisi ndogo ya Makao Makuu Dar es Salaam ikiwemo wanafunzi kutoka vyuo na shule mbalimbali za sekondari;
- v. Kufanya utafiti kuhusu kiwango cha wateja kuridhika na huduma zitolewazo na Mamlaka ambapo matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa wateja wa nje wanaridhika kwa 80% ilhali kiwango cha kulidhika kwa wateja wa ndani ni 75%;
- vi. Kupokea na kushughulikia hoja za wateja ambapo hoja 45 kuhusu usalama wa dawa na vifaa tiba katika soko zilipokelewa na kufanyiwa kazi.

### 2.4 KUIMARISHA UWEZO WA MAMLAKA KATIKA KUTOA HUDUMA ZA UDHIBITI

Ili Mamlaka iweze kutoa huduma bora za udhibiti, haina budi kuimarisha uwezo wake hususan kwa kuwa na

vitendea kazi mbalimbali ikiwemo majengo ya ofisi na maabara, magari, vifaa vya TEHAMA, kuongeza idadi ya watumishi na kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na hatimaye kuweza kugharamia shughuli zote za udhibiti kwa mujibu wa Sheria. Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Juni, 2021 kazi mbalimbali zilitekelezwa chini ya Lengo Mkakati hili kama ilivyoainishwa katika vipengele 2.4.1 – 2.4.9.

#### 2.4.1 Usimamizi wa rasilimali watu

Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Juni, 2021 kazi zilizofanyika katika eneo la usimamizi wa rasilimali watu na utawala zimeainishwa katika vipengele 2.4.1.1 - 2.4.1.2.

##### 2.4.1.1 Ajira

Mamlaka ilipokea watumishi 34 (33 waliohamia/kuazimwa kutoka katika taasisi nyingine za Serikali na mmoja ajira mpya) na hivyo kufanya jumla ya watumishi wa ajira ya kudumu kuwa 278. Aidha, Mamlaka iliajiri watumishi 18 wa mkataba wa mwaka mmoja baada ya kupokea kibali kutoka kwa Katibu Mkuu (UTUMISHI) hivyo kufanya jumla ya watumishi wa mkataba kuwa 50.

Vilevile katika kipindi hiki kati ya watumishi 92 waliotakiwa kupandishwa vyeo, Mamlaka ilifanikiwa kupandisha vyeo watumishi 82 waliokidhi vigezo na watumishi watano (5) kubadilishwa kada.

##### 2.4.1.2 Utekelezaji wa mpango wa mafunzo

Kwa mujibu wa mpango wa mafunzo wa Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2020/2021 watumishi 88 walipendekezwa kuhudhuria mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi. hadi kufikia Juni, 2021 watumishi 67 sawa na 76% walihudhuria kama inavyooneshwa katika Jedwali Na.14. Aidha Mamlaka iliendesha mafunzo maalum ya uongozi na utawala kwa Wakurugenzi na Mameneja 23 ikiwa ni utekelezaji wa mpango tajwa.





## JEDWALI NA 14: IDADI YA WATUMISHI WALIOHUDHURIA MAFUNZO YA AINA MBALIMBALI

Na.	Aina ya mafunzo	Waliopendekezwa	Waliohudhuria	(%) waliohudhuria
1.	Mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi	26	22	85
2.	Mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi	35	31	89
3.	Mafunzo ya muda mrefu nje ya nchi	12	10	83
4.	Mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi	15	4*	27
<b>Jumla</b>		<b>88</b>	<b>67</b>	<b>76</b>

\* Ushiriki wa mafunzo hayo uliathiriwa na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19

### 2.4.2 Uhakiki mifumo na usimamizi wa vihatarishi

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21, Mamlaka ilitekeleza kazi za uhakiki mifumo na usimamizi wa vihatarishi kama ifuatavyo:-

- Kusimamia zoezi la ukaguzi wa nje wa mfumo wa uhakiki ubora wa huduma, ambapo Mamlaka ilikaguliwa na kupewa cheti cha ISO 9001:2015 kwa mara ya nne (4) tangu mwaka 2009 kuthibitisha uwepo wa mfumo thabiti wa uhakiki ubora wa huduma.
- Kuandaa, kufanyia mapitio na kusambaza kwa wahusika jumla ya nyaraka 148 zikiwemo kanuni, miongozo, taratibu sanifu za utendaji kazi (SOPs), michakato na fomu mbalimbali za kusaidia utekelezaji wa majukumu.
- Kufanya kikao cha 13 cha Menejimenti cha mapitio ya Mfumo wa Uhakiki Ubora wa Huduma ikiwa ni moja ya takwa la kiwango cha ISO 9001:2015.
- Kufanya ukaguzi wa ndani wa mfumo wa uhakiki ubora wa huduma ambapo ofisi zote za kanda, vitengo na sehemu zilikaguliwa na mapungufu kufanyiwa kazi.
- Kufanya mapitio ya rejesta ya vihatarishi vinavyoweza kuathiri malengo ya kimkakati na kuandaa mpango kazi wa kutibu jumla ya vihatarishi 21.
- Kufanya tathmini na uchambuzi wa vihatarishi 16 vya udanganyifu (fraud risks) na kuandaa rejesta na mpango kazi wa kuvitibu.
- Kufanya tathmini na uchambuzi wa vihatarishi vinavyoweza kuathiri malengo ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi za kanda katika ngazi ya targets na kuandaa rejesta na mpango kazi wa kuvitibu.
- Kufanya tathmini ya mfumo wa usimamizi wa vihatarishi kwa kutumia nyenzo maalum ya kupima kiwango cha ukomavu cha usimamizi wa vihatarishi (risk maturity assessment matrix) na kuanisha maeneo yanayohitaji maboresho.

- Kutoa mafunzo ya uelewa kwa viongozi na watumishi wa Mamlaka kuhusu mfumo wa uhakiki ubora wa huduma na mfumo wa usimamizi wa vihatarishi ili kuleta ufanisi wa utekelezaji.

### 2.4.3 Ukaguzi wa Ndani

Katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Juni, 2021 kazi zilizofanyika na kukamilika ni zifuatazo: -

- Ufuatiliaji wa utekelezaji wa hoja za kaguzi za Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali (IAG) na Ukaguzi wa Ndani;
- Mapitio ya hati za malipo na masurufu, mishahara, mapitio ya usawazishaji wa vitabu vya Mamlaka na Akaunti za Benki, ukaguzi wa manunuzi, ukaguzi wa usimamizi wa mali za Mamlaka,

Ukaguzi wa mikopo kwa watumishi, ukaguzi wa mfumo wa RIMS, mapitio ya mpango wa uendelezaji huduma (BCP) wa Mamlaka, ukaguzi wa mradi wa ujenzi wa jengo la TMDA – Dodoma, mapitio ya mfumo wa usajili wa bidhaa za dawa, mapitio ya mpango wa ufuatiliaji wa ubora wa vifaa tiba na vitendanisha sokoni (PMS), mapitio ya Sehemu ya Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini, ukaguzi wa Ofisi za Kanda, kuandaa Mpango kazi wa ukaguzi wa ndani wa mwaka 2021/22 na kushiriki katika kazi ya uhakiki wa mali za Mamlaka.

Kwa ujumla kaguzi zilibaini kuwa kuna uzingatiaji wa taratibu za fedha, manunuzi na miongozo mbalimbali ya utendaji kazi. Mapendekezo stahiki yalitolewa kwa maeneo yenye upungufu ili yafanyiwe kazi kwa lengo la kuboresha mifumo.

### 2.4.4 Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

Mamlaka katika kuboresha na kutoa huduma kwa kutumia mfumo wa TEHAMA ilitekeleza kazi mbalimbali kama zilivyoainishwa katika **Jedwali Na.15.**

## JEDWALI NA. 15: MCHANGANUO WA KAZI ZA TEHAMA

Na.	Kazi zilizopangwa	Utekelezaji
1	Uboreshaji wa mfumo wa huduma za kiudhibiti unaojulikana kama <i>Regulatory Information Management System (RIMS)</i>	a) Mfumo umewezesha upokeaji wa maombi ya wateja kwa njia ya mtandao; b) Mfumo unawezesha wateja kufuatilia maombi yao kirahisi kwa njia ya mtandao; na c) Taarifa zimeboreshwa na hivyo kusaidia katika ufanyaji wa maamuzi sahihi.
2	Kusimamia na kufanya majaribio na utumiaji wa mfumo wa utoaji wa mizigo katika vituo vya forodha wa pamoja unaojulikana kama <i>Tanzania Electronic Single Window System</i>	Mfumo wa <i>Single window</i> umeweza kufanyiwa majaribio ya kina, na hivi sasa umeweza kutumika rasmi. Mfumo huu umeweza kudhibiti Wateja kudanganya thamani ya mizigo. Aidha mfumo umesaidia kuthibiti wateja kukwepa tozo na ukaguzi wa TMDA.
3	Uhakiki wa mfumo <i>Laboratory Information Management System (LIMS)</i>	Mfumo wa LIMS ulifanyiwa marejeo na kuboreshwa (validation) ili kukidhi mahitaji ya vigezo vya Shirika la Afya Duniani (WHO) na vya Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA).
4	Vifaa vipya vya TEHAMA	<i>Laptops 15, Server 2, Storage facilities 2, Printer 7, scanner 4</i> zilinunuliwa, kukaguliwa na kugawiwa kw. watumishi kwa ajili ya matumizi.
5	Kutoa msaada wa kiufundi katika ofisi za Kanda	Msaada wa kiufundi ulitolewa katika ofisi zote za Kanda. Pia mafunzo yalifanyika kwa watumishi wote wa ofisi ndogo ya makao makuu na ofisi za Kanda ambayo yalihusu mfumo mpya wa RIMS na usalama wa mfumo ya TEHAMA
6	Ukamilishaji wa uhakiki wa mfumo wa LIMS	Mfumo wa LIMS ulihakikiwa ambapo taarifa ya uhakiki iliandaliwa.
7	Utekelezaji wa ubora wa Mkataba wa huduma ya vifaa vya TEHAMA. (Kompyuta Maintenance)	Mamlaka ikishirikiana na Mzabuni iliweza kupitia ubora wa vifaa na kufanya matengenezo kwa vifaa vyenye hitilafu. Matengenezo haya yalihusu Kompyuta, <i>Photocopiers, UPS, scanner, printers.</i>
8	Usimikaji wa leseni za mfumo wa kulinda usalama wa taarifa (Ant-Virus installation)	Mamlaka imeweza kusimika leseni za kulinda usalama wa taarifa katika kompyuta zote za mamlaka na ofisi zote za Kanda

### 2.4.5 Ununuzi na Ugavi

Mamlaka ilisimamia utekelezaji wa Mpango wa Manunuzi wa mwaka 2020/21 ili kuwezesha upatikanaji wa vifaa na huduma mbalimbali zitakazowezesha kazi za udhibiti kufanyika kwa ufanisi.

Kulingana na Mpango uliopitishwa, Mamlaka ilipanga kufanya Manunuzi yenye gharama ya TZS 4,270,212,000.00. Hata hivyo, baada ya utekelezaji wa Mpango kufanyika, jumla ya mikataba ya manunuzi 31 yenye thamani ya TZS 3,393,363,396.67 ilitolewa kwa wazabuni mbalimbali. Kati ya mikataba iliyotolewa, mikataba 23 yenye thamani ya TZS 3,257,222,856.63 imekamilika ili hali mikataba 8 yenye thamani ya TZS 136,140,540.04 ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 16.

**Mamlaka ilisimamia utekelezaji wa Mpango wa Manunuzi wa mwaka 2020/21 ili kuwezesha upatikanaji wa vifaa na huduma mbalimbali zitakazowezesha kazi za udhibiti kufanyika kwa ufanisi.**

## JEDWALI NA 16: UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MANUNUZI KWA KIPINDI CHA 01 JULAI, 2020 HADI 30 JUNI, 2021

Na.	Utekelezaji	Idadi	Gharama halisi (TZS)
1	Mikataba iliyotolewa	31	3,393,363,396.67
2	Mikataba iliyokamilika	23	3,257,222,856.63
3	Mikataba inayoendelea	08	136,140,540.04
4	Zabuni zilizopitishwa kwenye Mpango	31	4,270,212,000.00

### 2.4.5.1 Mafanikio katika kusimamia Mpango wa Manunuzi wa mwaka 2021

Mpango wa manunuzi ulitekelezwa kwa mafanikio makubwa ambapo vifaa na huduma mbalimbali vilinunuliwa kwa mahitaji ya ofisi kama ifuatavyo;

- Kukamilisha ujenzi wa jengo la ofisi ya TMDA, Dodoma;
- Magari mawili aina ya Coaster na Hiace yalinunuliwa ili kurahishisha kazi za shughuli za uhibitaji;
- Mafuta ya magari na mitambo;
- Vifaa na kemikali mbalimbali za maabara;
- Samani za ofisi;
- Matengenezo ya vifaa vya Maabara, Vifaa vya TEHAMA, mitambo na magari; na
- Huduma za viburudisho, mtandao, usafi na Ulinzi.

### 2.4.6 Usimamizi wa Sheria

Katika kuhakikisha kwamba Mamlaka inafanya kazi kwa mujibu wa sheria, jumla ya vikao vinne (4) vya kawaida na kimoja (1) cha dharura vya Bodi ya Ushauri ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (MAB) kwa Mamlaka vilifanyika. Vikao hivi, vililenga kusimamia masuala mbalimbali ya kimkakati na kisera yaliyohusu utendaji wa Mamlaka kama ulivyoidhinishwa kwenye Mpango Mkakati wa miaka mitano pamoja na mpango kazi na bajeti wa mwaka 2020/21.

Mashauri ya madai mawili (2) ya fidia dhidi ya Mamlaka yalimalizika katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam. Katika Mashauri hayo, zaidi ya TZS billion 210 kabla ya kujumuisha riba za kibenki ambazo Mamlaka ingelipa kama fidia

**Vilevile kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka pamoja na Jeshi la Polisi nchini Mamlaka iliendesha kesi 103 za jinai kutokana na uvunjaji wa sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219 katika vituo vya Polisi na Mahakama mbalimbali nchini.**

ziliweza kuokolewa pamoja na TZS milioni 100 zilizokuwa zikidaiwa kama fidia na baadhi ya wamiliki wa maduka ya dawa muhimu nchini.

Madai haya ni pamoja na yale yaliyofunguliwa Mahakamani tangu mwaka 2013 yakidai kufidia hasara iliyodaiwa kusababishwa na hatua ya Mamlaka kukifunga kwa mwaka mmoja kiwanda cha kuzalisha dawa cha Arusha (TPI) kwa tuhuma za kusambaza dawa bandia za kufubaza virusi vya ukimwi.

Vilevile kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka pamoja na Jeshi la Polisi nchini Mamlaka iliendesha kesi 103 za jinai kutokana na uvunjaji wa sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219 katika vituo vya Polisi na Mahakama mbalimbali nchini.

Kati ya hizo kesi 35 zilifungwa kwa watuhumiwa kupatikana na hatia na hatimaye kulipa faini na adhabu mbalimbali za kisheria, kesi 21 zinaendelea mahakamani na zingine 47 upelelezi unaendelea chini ya Jeshi la Polisi. Mchanganuo wa mashauri na majalada mbalimbali umeainishwa katika **Jedwali Na. 17.**

**JEDWALI NA 17: IDADI YA MAJALADA YA UPELELEZI NA KESI ZA JINAI HADI TAREHE 30 JUNI 2020/21**

Jina la Kanda	Zilizofunguliwa kwenye vituo vya Polisi	Zinazoendelea Mahakamani	Zilizokwisha	Zinazoendelea na Upelelezi
Mashariki-Dar es salaam	16	2	4	10
Ziwa-Mwanza	12	1	2	9
Kusini-Mtwara	11	0	7	4
Kaskazini-Arusha	26	3	13	10
Nyanda za Juu Kusini-Mbeya	10	6	2	2
Kati-Dodoma	7	4	2	1
Magharibi-Tabora	20	5	5	10
<b>Jumla kuu</b>	<b>103</b>	<b>21</b>	<b>35</b>	<b>47</b>

Kama sehemu ya uimarishaji wa miongozo ya kisheria, Mamlaka ilikamilisha Kanuni kumi na tano (15) chini ya Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219 ambapo kumi (10) kati ya hizo zilitangazwa katika Gazeti la Serikali na tano (5) zinatarajiwa kutangazwa kabla ya mwezi Septemba 2021. Mchanganuo wa Kanuni, Miongozo na Sheria vilivyoandaliwa umeainishwa katika **Jedwali Na. 18**.

**JEDWALI NA 18: KANUNI, MIONGOZO/SERA NA SHERIA VILIVYOANDALIWA HADI TAREHE 30 JUNI, 2021**

NA	JINA LA KANUNI/MWONGOZO/ SHERIA	HATUA ILIYOFIKIWA
1	Kanuni za dawa za magonjwa yasiyopewa kipaumbele, 2018.	Inasubiri idhini na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali
2	Kanuni za usajiliwa majengo, uingizaji na usafirishaji wa dawa na malighafi nje ya nchi, 2015	
3	Kanuni za uondoaji katika soko, ushughulikiaji na uteketezaji wa dawa zisizofaa, 2015	
4	Mwongozo wa mafunzo kwa wakaguzi juu ya utimizaji wa matakwa ya kisheria	Imeanza kutumika
5	Kanuni za usambazaji na uhifadhi bora wa bidhaa za tiba	
6	Ada na Tozo	Nakala ya Kiswahili na kiingereza zote zinasubiri idhini na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali
7	Udhibiti wa Bei za Dawa	Inasubiri idhini na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali
8	Sheria Mpya ya TMDA, Sura 219	Hatua za kisera za idhini
9	Sheria Rejewa ya TMDA, Sura 219	Kusainiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali
10	Kutangaza Wakaguzi GN.257/20	Zinatumiwa
11	Kutangaza Wakaguzi GN.191/2020	
12	Kutangaza Wakaguzi GN.1009/2020	
13	Kutangaza Wakaguzi GN.190/2020	
14	Kudhibiti Bidhaa za Tumbaku, GN. 360/2021	
15	Kutangaza Wachunguzi wa Kimaabara GN.409/2021	
16	Kutangaza Dawa Zilizosajiliwa, GN. 187/2020	

